Muhtasari
Tanzania
Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu **2017**

Empowered lives.
Resilient nations.

United Republic of Tanzania

Sera ya Kijamii Katika Muktadha wa Mageuzi ya Kiuchumi

Muhtasari

Tanzania
Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu **2017**

Sera ya Kijamii Katika Muktadha wa Mageuzi ya Kiuchumi

Empowered lives.
Resilient nations.

United Republic of Tanzania

Implementing Partner

Tanzania Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu 2017
Sera ya Kijamii Katika Muktadha wa Mageuzi ya Kiuchumi

Hati ya Kumiliki © 2018

Kimeandaliwa na
Economic and Social Research Foundation (ESRF)
51 Uporoto Street (Barabara ya Ali Hassan Mwinyi),
Ursino Estates S.L.P 31226, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: (+255) 22 2926084, 2926085, 2926086, 2926087, 2926088, 2926089, 2926090
Simu ya Mkononi: +255-754 780133, +255-655 780233 Fax: +255-22 2926083
Nukushi: esrf@esrf.or.tz OR info@esrf.or.tz
Tovuti: http://www.esrf.or.tz, http://www.thdr.or.tz

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
Ofisi ya Tanzania
182 Mzinga way, Barabara ya Msasani, Oysterbay
S.L.P 9182, Dar es Salaam, Tanzania
Simu (+255) 22 2112576 +255 686 036 436

Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Tanzania:
Simu: +255 686 036 436 +255 686 036 436
Ofisi ya Mkurugenzi wa UNDP nchini Tanzania:
Simu: +255 0686 036 475 +255 0686 036 475
Barua pepe: registry.tz@undp.org
Tovuti: http://www.tz.undp.org

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Fedha na Mipango
Treasury Square Building
18 Jakaya Kikwete Road
P.O.Box 2802,
40468 Dodoma
Tel: +255 26 2963101
Tel: +255 26 2963109
Website: http://www.mof.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutoa sehemu ya chapisho hili, kuhifadhi au kuwasilisha katika umbo lolote au kwa namna yeyoteile, ki eletroniki, kwa kutumia mitambo, kunakili, kurekodi au vinginevyo bila idhini ya awali.

ISBN: 978-9976-5231-7-1

Mchoro katika ukurasa wa mbele umebuniwa na ndugu Haji Chilonga wa Dar es Salaam, Tanzania

Kimesanifiwa na kuchapishwa na Jamana Printers, Tanzania

DIBAJI

Ripoti ya kwanza ya Maendeleo ya Binadamu duniani (HDR), iliyotolewa mwaka 1990 na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) ilitoa mwongozo kwamba Maendeleo ya Binadamu yatazamwe kama njia mpya ya kuelewa na kukuza ustawi wa watu. Mtazamo wa ripoti hiyo ya kwanza ya Maendeleo ya Binadamu ulilenga kuiona dhana ya maendeleo kama "mchakato wa kupanua fursa za watu katika kufanya maamuzi". Kwa kuyafanya maisha ya watu kuwa chanzo kikuu cha fikra kuhusu maendeleo na uchumi, ripoti hiyo na nyingine zilizofuatia zilileta mageuzi makubwa ya mtazamo wa maendeleo na namna viongozi mbalimbali wa dunia wanavyozichukulia dhana za umaskini na ukosefu wa haki. Katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, Ripoti za Maendeleo ya Binadamu za dunia zimeambatana na zaidi ya dazeni tatu za ripoti za kanda kuu na kanda ndogondogo, na zaidi ya ripoti 700 za mataifa mbalimbali. Ripoti hizi ni zana za kimkakati zilizotengenezwa kupitia mchakato shirikishi ndani ya nchi na kanda katika kushughulikia na kuchanganua masuala muhimu ya watu. Ripoti hizi ni chanzo muhimu cha uvumbuzi na uboreshaji wa sera za maendeleo na utekelezaji wake.

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya Tanzania (THDR) ya mwaka 2017 ni ya pili kitaifa nchini Tanzania. Mada kuu ya ripoti ya mwaka huu ni "Sera ya Kijamii katika Muktadha wa Mageuzi ya Kiuchumi Nchini Tanzania" ambayo ilichaguliwa makusudi ili kuendeleza dhana zilizoibuliwa na Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya Tanzania ya mwaka 2014. Katika miaka ya karibuni, mkakati wa maendeleo ya kiuchumi nchini Tanzania umeweka mkazo kwenye umuhimu wa mageuzi ya kiuchumi katika kupunguza umaskini na kuleta ustawi. Dhana ya "mageuzi ya kiuchumi" inamaanisha mabadiliko katika muundo wa uchumi kuelekea katika uchumi ambao hautegemei sana sekta ya kilimo bali sekta za viwanda na huduma katika mchango wa Pato la Taifa, ikiambatana na mabadiliko ya idadi ya watu, kutoka kuwa na vizazi na vifo vingi hadi kuwa na vizazi na vifo vichache. Kutokana na umuhimu wa mageuzi ya kiuchumi ambayo Tanzania imedhamiria kuyafanya, Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2014 ilibeba mada ya "Mageuzi ya Kiuchumi kwa Maendeleo ya Binadamu". Ripoti hiyo ya mwaka 2014 ilijikita katika dhana kuu kwamba, ili mageuzi ya kiuchumi yalete maendeleo ya binadamu, mchakato wa mageuzi ni lazima uende sambamba na upatikanaji wa ajira, ongezeko la kipato na utoaji wa huduma za jamii. Hivyo, Ripoti hii ya mwaka 2017 imelenga kuendeleza fikra za ripoti iliyotangulia katika kuchambua nafasi ya sera ya kijamii na utoaji wa huduma za kijamii katika mchakato endelevu wa mageuzi ya kiuchumi nchini Tanzania.

Muundo wa muhtasari huu unaakisi muundo wa ripoti kuu. Muhtasari huu una sura nne na viambatisho vya takwimu. Sura ya kwanza inatoa picha ya hali ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania. Sura ya pili inajadili nafasi ya sera ya kijamii katika mageuzi ya kiuchumi. Sura ya tatu inaelezea historia ya muingiliano wa sera ya kijamii na kiuchumi tangu uhuru nchini Tanzania. Sura ya nne inatathmini changamoto zinazohitaji kutatuliwa na fursa zinazohitaji kutumiwa na serikali ya Tanzania katika kuifanya sera ya kijamii isijielekeze kwenye matokeo tu, bali pia iwe njia ya kuelekea kufanikisha mageuzi endelevu ya kiuchumi kwa maendeleo ya binadamu. Viambatisho vya takwimu vinatoa picha ya jumla ya viashiria vya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kibinadamu.

THDR 2017 imeandaliwa kwa msaada wa UNDP kupitia Mpango wa Maendeleo ya Binadamu, ambao ulilenga kuwatumia wataalamu wa ndani na kupata mrejesho kutoka kwa wahusika wa sera za mandeleo na mipango, ikijumuisha taasisi za serikali. Kwa kutumia msaada wa kifedha kutoka UNDP, uandaaji wa ripoti ulihusisha mtandao wa wataalamu kutoka taasisi za utafiti na vyuo vikuu. Asasi ya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii (ESRF) ilikuwa ndiye mtekelezaji mkuu wa mradi wa THDR ikishirikiana kwa karibu na taasisi kadhaa, zikiwemo Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (OCGS) na Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Meneja wa mradi na sekretarieti ya uandaaji wa ripoti hii walifanya kazi za kila siku za uandaaji kwa ushirikiano wa karibu na timu ya wataalamu kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Asasi ya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii (ESRF), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Vile vile, kikosi kazi kikubwa zaidi, kilichojumuisha wataalamu 35 kutoka katika taasisi mbalimbali za taifa na wakala za maendeleo, kilitoa msaada mkubwa, mrejesho na mwongozo katika kipindi chote cha uandaaji wa ripoti hii. Mchakato wa uandaaji ulihusisha kuwapa wataalamu kazi ya kuandika makala kumi na moja zilizochangia maudhui muhimu kwa ajili ya uandishi wa ripoti hii. Sambamba na hilo, ukusanyaji wa taarifa juu ya viashiria muhimu vya maendeleo ya binadamu ulifanyika ili kuandaa viambatisho vya takwimu. Tungependa kutoa shukrani zetu kwa waandishi wafuatao wa makala zilizochangia kuandikwa kwa ripoti hii ya Maendeleo ya Binadamu nchini Tanzania ya mwaka 2017:

Makala Na. 1: "Hali na Ukuaji wa Maendeleo ya Binadamu nchini Tanzania"
Prof. Haidari Amani, Dkt. Tausi Kida na Bw. Danford Sango.

Makala Na. 2: "Hali na Ukuaji wa Maendeleo ya Binadamu Zanzibar"
Dkt. Flora Kessy na Bi. Mashavu Omar

Makala Na. 3: "Mabadiliko ya Idadi ya Watu na Sera ya Kijamii"
Prof. Haidari Amani, Prof. Alfred Agwanda na Bw. Ahmed Makbel

Makala Na. 4: "Uwekaji wa Sera ya Kijamii katika Mageuzi ya Kijamii na Kiuchumi: Kiunzi cha Dhana.
Prof. Marc Wuyts na Dkt. Hazel Gray

Makala Na. 5: "Utegemezi wa Misaada katika kugharamia Utoaji wa Huduma za kijamii Nchini Tanzania: "Mtazamo wa Uchumi Mkubwa" Prof. Marc Wuyts, Bw. Desmond Mushi na Dkt. Tausi Kida

Makala Na. 6: "Sera ya Kijamii katika Mtazamo wa Kihistoria: Mabadiliko ya Mbinu katika Utoaji wa Huduma za Kijamii"
Dkt. Jehovaness Aikaeli na Prof. Humphrey Moshi

Makala Na. 7: "Sera ya Kijamii, Jinsia na Kazi"
Prof. Razack Lokina, Dkt. Joyce Nyoni na Prof. Godius Kahyarara

Makala Na. 8: "Afya kama Sekta ya Uzalishaji: kufungamanisha Sera ya Afya na Viwanda"
Prof. Maureen Mackintosh na Dkt. Paula Tibandebage

Makala Na. 9: "Hifadhi ya Jamii: Je, ni nyavu kwa ajili ya usalama au Nyenzo za kufanyia Mageuzi? "
Dkt. Flora Myamba na Dkt. Sheshangai Kaniki

Makala Na. 10: "Misingi ya Elimu kwa Maendeleo ya Ujuzi na Uzalishaji"
Prof. Suleman Sumra na Dkt. Joviter Katabaro

Makala Na. 11: "Maji, Usafi na Maji Taka Nchini Tanzania: Upatikanaji wa Huduma, Mwelekeo wa Sera na Ugharamiaji"
Dkt. Flora Kessy na Bw. Richard Mahali

Tungependa kumshukuru kwa dhati Dkt. Tausi Kida, Mkurugenzi Mtendaji wa ESRF, kwa uongozi, mwongozo wa kiufundi na uratibu wake katika mchakato wote wa kuandaa na kutoa ripoti hii. Shukrani maalum pia zimwendee Prof. Marc Wuyts (ISS) kwa mwongozo wake wa kitaaluma alioutoa katika mchakato wote. Shukrani za kipekee ziende pia kwa timu maalumu iliyoandaa ripoti hii kwa umakini wao. Sambamba na Dkt. Tausi Kida na Prof. Marc Wuyts, timu hii iliundwa pia na Bw. Amon Manyama (UNDP), Dkt. Jehovaness Aikaeli (UDSM), Dkt. Kenneth Mdadila (UDSM), Bw. Ahmed Markbel (Ofisi ya Waziri Mkuu), Bw. Irenius Ruyobya (NBS), Bw. Deogratias Mutalemwa (ESRF), Dkt. Hazel Gray (Chuo Kikuu cha Edinburgh, Uingereza), Prof. Samuel Wangwe (ESRF), Bw. Christian Shingiro (UNDP), Bi. Kristina Weibel (UNDP) na Dkt. Rogers Dhliwayo, Mshauri wa zamani wa uchumi wa UNDP nchini Tanzania.

Shukrani zetu za dhati ziende kwa timu iliyoandika ripoti ambayo ilijumuisha wataalamu wafuatao: Prof. Haidari Amani, Dkt. Tausi Kida na Bw. Danford Sango (Sura ya 1); Dkt. Hazel Gray (Sura ya 2); Prof. Samuel Wangwe, Dkt. Josaphat Kweka na Prof. Marc Wuyts (Sura ya 3); Prof. Samuel Wangwe na Dkt. Josaphat Kweka (Sura ya 4); na Dkt. Kenneth Mdadila na Bw. Irenius Ruyobya (viambatisho vya takwimu)1. Uandaaji wa viambatisho vya takwimu ulifanikiwa sana kutokana na msaada mkubwa kutoka Ofisi za Taifa za Takwimu za Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa msingi huo, tunapenda kuwashukuru Dkt. Albina Chuwa – Mkurugenzi Mkuu NBS – na Bi. Mayasa Mwinyi, Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa msaada wao katika uandaaji wa ripoti hii ya mwaka 2017.

Kwa kiasi kikubwa, maandalizi ya Ripoti hii ya Maendeleo ya Binadamu ya 2017 yalinufaika na mrejesho na mwongozo uliotolewa na kikosi kazi cha watu 35 wa Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu nchini Tanzania, ambapo wengi wao ni maafisa waandamizi kutoka katika taaluma na nyadhifa mbalimbali. Ofisi maalum zilizotoa wataalamu hao ni hizi zifuatazo: Bunge la Tanzania, Wizara ya Fedha na Mipango, Tume ya Mipango, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Taifa

[1] Maoni yaliyomo katika ripoti hii ni ya waandishi, na hayawakilishi maoni ya UNDP, Umoja wa Mataifa wala asasi yoyote inayohusiana na hizi.

ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), NBS, OCGS, UNDP, ESRF, UDSM, REPOA, Taasisi ya UONGOZI, Shirika la Kazi Duniani (ILO), Benki ya Dunia, Shirika la Afya Duniani (WHO), UNICEF, Jukwaa la Utu wa Watoto, na Shirika la Kimataifa la Kusaidia Wazee. Tungependa pia kutoa shukurani kwa wajumbe wa kikosi kazi cha uandaaji wa ripoti kwa msaada wao usio na kikomo katika kipindi chote cha uandaaji wa ripoti hii. Tungependa pia kumshukuru Bw. Jonathan Hall kutoka Ofisi ya Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu (HDRO) kwa msaada wa kitaaluma na mwongozo.

Pia, tunawashukuru Bw. Danford Sango (ESRF) na Bw. Yasser Manu (ESRF) kwa mchango wao wa kiufundi na kiutawala kama wanatimu wa sekretarieti ya THDR. Tungependa pia kumshukuru Bi. Margareth Nzuki na timu nzima ya Menejimenti ya Ujuzi ya ESRF kwa msaada wao katika kusambaza ripoti hii. Tunamshukuru pia Bw. Chris Daly, Mshauri Mkuu, kwa uhariri wa muswada wa mwisho. Tunatoa shukurani zetu pia kwa Bw. Nicolai Schulz kwa mchango wake kwenye muhtasari wa ripoti na Dkt. Rashid Chuachua kwa kutafsiri muhtasari huu kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili. Shukurani za pekee pia tunazielekeza kwa msanii wa Kitanzania, Bw. Haji Chilonga, kwa usanifu wa jalada la ripoti hii.

Mwisho kabisa tunashukuru busara na mwongozo wa Mh. Dkt. Ashatu K. Kijaji, Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango katika kipindi chote cha Kongamano la Tano la Kitaifa la ESRF lililokuwa na kichwa "Sera ya Kijamii katika Muktadha wa Mageuzi ya Kiuchumi nchini Tanzania" lililofanyika tarehe 29 Novemba 2016. Mada kuu ya kongamano hilo la kitaifa ilipata msukumo wa Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2017, na kongamano hilo lilijumuisha uwasilishaji wa mada na majadiliano kuhusu makala 11 za ripoti.

Kutokana na juhudi hizi, tuna matumaini makubwa kuwa ripoti hii itatoa uelewa mpana kwa wasomaji juu ya nafasi muhimu ya sera ya kijamii katika kufanikisha mageuzi ya kiuchumi kwa maendeleo ya binadamu nchini Tanzania.

Bw. Doto Mgosha James
Katibu Mkuu,
Wizara ya Fedha na Mipango,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Bw. Alvaro Rodriguez
Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN)
na Mwakilishi Mkazi wa UNDP Nchini
Tanzania

Yaliyomo

Dibaji	iii
Yaliyomo	vi
Vifupisho vya maneno	vii
Utangulizi	viii

SURA YA 1

Hali na ukuaji wa maendeleo ya binadamu Tanzania	1
Tanzania na Mpango wa Maendeleo ya Binadamu	1
Matokeo ya viashiria muhimu vya maendeleo ya binadamu	1
Vichocheo vya Maendeleo ya Binadamu Nchini Tanzania: Matokeo ya Utafiti kuhusu Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu na Kipimo cha Umaskini wa Namna Tofauti	6
Mabadiliko ya idadi ya watu na maendeleo ya binadamu nchini Tanzania	10

SURA YA 2

Dhima ya sera ya kijamii katika mageuzi ya kiuchumi	13

SURA YA 3

Kufungamanisha sera za kiuchumi na za kijamii - msisitizo unaobadilika katika mwongozo wa sera ya taifa tangu uhuru	16
Uhuru hadi Azimio la Arusha (1961-66)	16
Azimio la Arusha hadi mdororo wa kiuchumi (1967-1985)	16
Marekebisho na Mabadiliko ya Mfumo wa Kiuchumi (1986 hadi 1996)	18
Kudai tena Udhibiti wa ajenda ya Maendeleo ya Taifa (1996-2016)	18

SURA YA 4

Sera ya jamii kama njia na lengo la mageuzi ya kiuchumi kwa maendeleo ya binadamu: Ujumbe muhimu katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya pili	20
Hitimisho	23
Marejeleo	24

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Mpangilio wa Mikoa Tanzania Bara kwa alama za ndani za HDI, 2015	2
Kielelezo Na. 2: Hesabu ya viwango vya umaskini katika mikoa ya Tanzania Bara, 2015, kulingana na mchanganuo wa Alama za ndani za MPI	3
Kielelezo Na. 3: Mikoa ya Tanzania Bara, kwa mgawanyo wa Alama za ndani za MPI, 2015	4
Kielelezo Na. 4: Hesabu ya uwiano wa kipato cha maskini katika mikoa ya Tanzania Bara, 2012	5
Kielelezo Na. 5: Mwelekeo na Malengo ya Pato la Mtu Mmoja Mmoja, 2007 hadi 2025	7
Kielelezo Na. 6: Mwelekeo wa Vifo vya Watoto Tanzania, vifo vya watoto chini ya miaka mitano na vichanga, 1990 hadi 2016	8
Kielelezo Na. 7: Huduma ya choo kwenye kaya (% ya kaya)	10
Kielelezo Na. 8: Idadi ya watu nchini Tanzania (1948–2035)	11
Kielelezo Na. 9: Mgawanyo wa idadi ya watu katika kaya nchini Tanzania kwa Umri-jinsi, 2012	11
Kielelezo Na. 10: Vipengele vya msingi vya hifadhi za jamii nchini Tanzania	14

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali na. 1: Umri wa kuishi tangu kuzaliwa Tanzania, 2002 na 2012	7

Vifupisho vya maneno

AIDS	Acquired Immune Deficiency Syndrome
DCF	Development Cooperation Framework
DHS	Demographic and Health Survey
DPs	Development Partners
ESR	Education for Self-Reliance
ESRF	Economic and Social Research Foundation
EYS	Expected Years of Schooling
FYDP	Five Year Development Plan
GDI	Gender Development Index
GDP	Gross Domestic Product
GII	Gender Inequality Index
GNI	Gross National Income
GoT	Government of Tanzania
HDI	Human Development Index
HIV	human immunodeficiency virus
IFIs	international financial institutions
ILO	International Labour Organization
IMR	Infant Mortality Rate
LTPP	Long Term Perspective Plan
MIS	Malaria Indicator Survey
MOFP	Ministry of Finance and Planning
MPI	Multidimensional Poverty Index
MYS	Mean Years of Schooling
NBS	National Bureau of Statistics
NER	Net Enrolment Rate
NESP	National Economic Survival Programme
OPHI	Oxford Poverty and Human Development Initiative
PRSPs	Poverty Reduction Strategy Papers
PSLE	Primary School Leaving Examination
PSPF	Public Service Pension Fund
RGoZ	Revolutionary Government of Zanzibar
SAP	Structural Adjustment Programme
TACAIDS	Tanzania Commission for AIDS
TDV	Tanzania Development Vision
U5MR	Under-Five Mortality Rate
US	United States
USD	United States dollar

Utangulizi

Mpango wa Maendeleo ya Binadamu na Viashiria Muhimu

Mwaka 1990, Ripoti ya kwanza ya Maendeleo ya Binadamu duniani ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) iliwasilisha Mkabala wa Maendeleo ya Binadamu (HDA) kama njia mpya ya kufahamu na kuinua ustawi wa binadamu. Mtazamo huu unaona kwamba maendeleo ni mchakato wa kupanua uhuru wa watu na kuimarisha uwezo wao, kulingana na nadharia ya kuendeleza uwezo ya Amartya Sen (Sen 1999). Hii inawahamasisha watunga sera kuutazama umaskini kwa upana zaidi ya kipimo cha kipato, na hivyo, kuvipa uzito mkubwa vitu ambavyo watu wenyewe wanavithamini sana.

Ili kupima, kulinganisha na kuchanganua mwelekeo wa matokeo ya maendeleo ya binadamu ndani na nje ya nchi, ripoti ya mwaka 1990 iliwasilisha Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI).2 HDI kinapima maendeleo yaliyofikiwa na nchi katika maeneo makuu matatu ya maendeleo ya binadamu:

Maisha bora na marefu, kwa kuzingatia umri wa kuishi tangu kuzaliwa;

Ujuzi, kwa kuzingatia viashiria viwili vya elimu yaani makadirio ya miaka ya masomo (EYS) na wastani wa miaka ya masomo (MYS); na

Kiwango cha ubora wa maisha, kwa kuzingatia pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja.

Mwaka 1995, Kipimo cha Maendeleo ya Jinsia (GDI) kilitambulishwa ili kuwezesha kupima Maendeleo ya Binadamu kwa mgawanyo wa jinsia.

Katika kupanua mchanganuo wa maendeleo ya binadamu na kukabiliana na vikwazo katika Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu na kipimo cha Maendeleo ya jinsia, Ripoti ya Mandeleo ya Binadamu ya UNDP ya mwaka 2010 ilitambulisha Kipimo cha Umaskini kwa Vigezo Mbalimbali (MPI) na Kipimo cha Tofauti za Kijinsia (GII). MPI huangalia viashiria kumi vya maendeleo ya binadamu kupitia maeneo matatu kama ya HDI ambayo ni afya, elimu na viwango vya maisha. Mtu atatambulika kuwa ni "maskini kwa mtazamo wa MPI" ikiwa atakuwa na theluthi moja au zaidi kati ya viashiria hivyo kumi; na atatambulika kuwa ni "maskini sana" ikiwa mtu huyo atakuwa na asilimia 50 au zaidi ya viashiria hivyo kumi. Kwa kuainisha watu walio katika umaskini mkubwa, kwa maana ya kuwa na viashiria vingi vya umaskini, MPI inaweza kuchangia kuhusu uandaaji wa sera na mipango na mgawanyo sahihi wa rasilimali. Vivyohivyo, GII iliandaliwa ili kudhibiti tofauti za jinsia katika maendeleo ya binadamu kwa kuangalia vigezo vikuu vitatu vya ustawi wa wanawake ambavyo ni: afya ya uzazi, uwezeshwaji (ambayo inajumuisha upataji wa elimu na uwakilishi wa kisiasa katika ngazi ya kitaifa) na ushiriki wao katika soko la ajira.

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu Tanzania (THDR) 2017

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2017 ni ya pili ya kitaifa nchini Tanzania. Mada kuu ya ripoti hii ni "Sera ya Kijamii katika Muktadha wa mageuzi ya kiuchumi nchini Tanzania". Kama ilivyokuwa katika ripoti ya uzinduzi ya mwaka 2014, sura ya utangulizi inaonyesha hali ya sasa ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania. Kwa kuzingatia taarifa za karibuni zaidi zilizopo, matokeo kwa vipimo vikuu vinne vya maendeleo ya binadamu (HDI, MPI, GDI na GII) vinawakilishwa kwa Tanzania Bara (na mikoa yake) na Zanzibar. Idadi ya maskini kutokana na tafiti za matumizi ya kaya za hivi karibuni pia zimejadiliwa. Kisha, ripoti hii inachanganua viashiria vilivyotumika kukokotoa HDI na MPI ili kuweza kutathmini kwa karibu masuala yanayosukuma matokeo ya maendeleo ya binadamu nchini. Ripoti hii inajadili pia uhusiano uliopo baina ya mabadiliko ya idadi ya watu nchini, hasa katika ongezeko la watu na ukuaji wa miji, na maendeleo ya binadamu.

---

[2] Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) hupima kiwango cha maendeleo ya nchi kwa kuanzia na 0 kwa kiwango cha chini cha Maendeleo ya Binadamu hadi 1 kwa kiwango cha juu cha Maendeleo ya Binadamu.

Zikijenga katika uchambuzi wa Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2014 ambayo ilijikita katika "Mageuzi ya Kiuchumi kwa Maendeleo ya Binadamu", sura kuu tatu za ripoti ya mwaka huu zinajadili dhima na nafasi ya sera ya kijamii katika mchakato unaoendelea wa mageuzi ya kijamii na kiuchumi. Sura ya pili inazungumzia nadharia ya uhusiano uliopo kati ya sera ya kijamii na kiuchumi katika kufanikisha mageuzi ya kiuchumi sanjari na maendeleo ya binadamu. Sura ya tatu inatoa mtazamo wa kihistoria kuhusu mwingiliano wa sera ya kijamii na za kiuchumi katika sera za Tanzania tangu nchi ilipopata uhuru. Katika kuhitimisha ripoti, sura ya nne na ya mwisho inatathmini changamoto zinazohitaji kutatuliwa na fursa zinazohitajika kupiganiwa na serikali ya Tanzania katika kuandaa sera ya kijamii ambayo haitajali matokeo pekee, bali itakuwa njia ya kuelekea kwenye kufanikisha mageuzi endelevu ya kiuchumi pamoja na maendeleo ya binadamu. Kwa ushawishi mkubwa, ripoti hii inajenga hoja kwamba, ili Tanzania iweze kufikia lengo la maendeleo iliyojiwekea na kuwa nchi ya viwanda, na ya kipato cha kati kufikia mwaka 2025, itahitaji mkakati mzuri wa kuoanisha sera za kiuchumi na zile za kijamii.

1.

Hali na ukuaji wa maendeleo ya binadamu Tanzania

Tanzania na Mpango wa Maendeleo ya Binadamu

Tangu uhuru, suala la maendeleo ya binadamu limekuwa kiini cha mchakato wa maendeleo nchini Tanzania. Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanzania, aliainisha umaskini, ujinga na maradhi kuwa ndio maadui wakuu wa maendeleo nchini Tanzania. Yeye alielewa maendeleo kama mchakato wa kutokomeza unyonge, na alijenga hoja kuwa uhuru na maendeleo ni mambo yaliyofungamana kwa namna zote (Nyerere 1973). Kimsingi, Nyerere na Sen wanakubaliana kuwa maendeleo lazima yawe ya watu, na yanapaswa kuimarisha uwezo wa watu ili kuwasaidia kuishi maisha marefu na toshelevu kwa kuwa na afya, elimu, maisha bora.

Katika kipindi cha muongo wa kwanza baada ya uhuru, sera rasmi ilisisitiza mtazamo wa Nyerere kuhusu maendeleo ya binadamu, ambao unaonyesha kwamba kwa muda mrefu Tanzania imefafanua dhana ya maendeleo ya taifa katika namna inayoendana na mpango wa maendeleo ya binadamu uliotolewa na Amartya Sen na kusimamiwa na UNDP tangu mwaka 1990. Leo, zaidi ya miaka 50 baada ya uhuru, mpango wa taifa wa maendeleo wa miaka mitano nchini Tanzania 2016/17-2020/21 (FYDP II) unalenga kufanikisha ukuaji wa viwanda ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu lengo kuu likiwa kuharakisha ukuaji kuelekea Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 (JMT 1999 na 2016a). Mpango huu unatambua wazi mahusiano yaliyopo baina ya maendeleo ya binadamu na ukuaji wa kiuchumi. Kwa kuzingatia hoja ya msingi kuwa ukuaji wa kiuchumi ni muhimu lakini haitoshelezi kuwa sababu pekee ya maendeleo, FYDP II inatilia mkazo umuhimu wa mabadiliko ya muundo wa viwanda kwa maendeleo ya binadamu. Chini ya mpango huu, serikali inalenga kuboresha alama za HDI kufikia 0.600 kwa mwaka 2025/26. Ripoti hii ya Maendeleo ya Binadamu Tanzania ya mwaka 2017 inachanganua hali ya sasa ya maendeleo ya binadamu nchini ili kutoa mwongozo kwa watunga sera kufikia lengo lililokusudiwa. Ufuatao ni muhtasari wa matokeo ya utafiti wa vipimo muhimu vya maendeleo ya binadamu pamoja na matokeo ya utafiti kuhusu viashiria vinavyosukuma matokeo ya maendeleo ya binadamu nchini Tanzania.

Matokeo ya viashiria muhimu vya maendeleo ya binadamu

Tanzania imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya binadamu, maendeleo ambayo yanathibitishwa na kuongezeka kwa alama za Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) kutoka 0.371 mwaka 1985 hadi 0.531 kwa mwaka 2015 ambalo ni ongezeko la asilimia 43.1 kwa kipindi cha miaka 30 (UNDP 2016). Kwa kuzingatia alama za mwaka 2015, Tanzania imepanda daraja ambalo ni zaidi ya wastani wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambayo ni 0.518. Hata Hivyo, Tanzania bado inabakia kwenye kundi la nchi zenye kiwango kidogo cha maendeleo ya binadamu, ambapo inashika nafasi ya 151 kati ya nchi 188 duniani. Tafiti zaidi za ndani zinaonyesha kuwa tofauti ya kimkoa ndani ya nchi ina mchango mkubwa pia. Kwa mfano, thamani ya HDI inatofatiana kwa kiwango cha juu cha 0.75 katika mkoa wa Kilimanjaro hadi kiwango cha chini cha 0.44 katika mkoa wa Kagera (Kielelezo Na. 1).

Kielelezo Na. 1:

Mpangilio wa Mikoa Tanzania Bara kwa alama za ndani za HDI, 2015



Chanzo: Imekokotolewa kwa ajili ya THDR 2017 kwa kuzingatia matokeo ya tafiti kutoka vyanzo na miaka tofauti. Kwa maelezo zaidi, tazama Jedwali A2 katika viambatisho vya kitakwimu katika ripoti kuu.

Matokeo ya Kipimo cha Umaskini wa kwa vigezo mbali mbali (MPI) yanaoana na yale ya Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu cha HDI; viwango vya umaskini kwa kutumia kipimo kinochojumuisha vigezo mbali mbali vimeshuka ingawa bado viko juu.3 Uwiano wa idadi ya watu wanaokabiliwa na umaskini kwa kutumia kipimo cha MPI umeshuka kutoka asilimia 64 mwaka 2010 hadi asilimia 47.4 mwaka 2015, na umaskini uliokithiri umeshuka kutoka asilimia 31.3 mwaka 2010 hadi asilimia 17.7 mwaka 2015. Mafanikio haya yametokana na ukweli kwamba Tanzania imeweza kufanya maboresho katika viashiria vyote vya MPI katika kipindi hiki. Hata Hivyo, ongezeko la upatikanaji wa umeme pamoja na umiliki wa rasilimali (zikiwemo simu za mkononi, redio na pikipiki) ni hoja

[3] Thamani ya Kipimo cha Umaskini wa Namna Tofauti (MPI) ilikokotolewa kwa kuzingatia data za Tanzania Demographic and Health Survey (TDHS) 2010 (NBS na ICF Macro 2011), pamoja na zile za Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015-16 (MoHCDGEC na Wenzake. 2016).

muhimu za kuelezea kushuka kwa umaskini kwa kigezo cha MPI kati ya mwaka 2010 na 2015. Mwelekeo huu unaendana na Malengo ya Taifa kama yalivyooneshwa kwenye FYDP II, kupunguza MPI kwa asilimia 38.4 kufikia mwaka 2020/21, na hatimaye, asilimia 29.2 kufikia mwaka 2025/26. Kadhalika, tofauti muhimu za kimikoa zinaendelea kuwapo. Kwa upande mmoja wa kipimo, asilimia 66 ya watu mkoani Rukwa inaishi katika umaskini kwa kipimo cha umaskini kwa vigezo mbali mbali (MPI) ikilinganishwa na asilimia 12 ya watu wa mkoa wa Dar es Salaam (tazama Kielelezo na. 2). Kwa upande wa Zanzibar, matokeo ya tafiti yanaonyesha kuwa uwiano wa kipimo cha umaskini kwa kutumia kipimo cha MPI umeshuka kutoka asilimia 43.3 mwaka 2010 hadi asilimia 26.3 mwaka 2015; na umaskini uliokithiri umeshuka kwa kiwango cha nusu yake kutoka asilimia 16.6 hadi asilimia 8.5 kwa kipindi hichohicho.

Kielelezo Na. 2:

Hesabu ya viwango vya umaskini katika mikoa ya Tanzania Bara, 2015, kulingana na mchanganuo wa Alama za ndani za MPI



Chanzo: Imekokotolewa kwa ajili ya THDR 2017 kulingana na matokeo ya Utafiti Idadi ya Watu na Afya Tanzania na Utafiti wa Viashiria vya Malaria (TDHS-MIS) 2015-16. Kwa maelezo zaidi, tazama Jedwali na. A5 katika viambatisho vya kitakwimu katika ripoti kuu.

Ili kuonyesha mgawanyo wa kijiografia wa matokeo ya maendeleo ya watu nchini Tanzania, alama za mikoa za Kipimo cha Umaskini cha MPI ziligawanywa katika viwango vitatu vya maendeleo ya binadamu ambavyo ni kiwango chini, cha kati na cha juu (tazama Kielelezo na. 3). Ramani ifuatayo inaonyesha kwamba maendeleo ya binadamu nchini Tanzania yana mgawanyiko wa kimaeneo ambapo baadhi ya maeneo yana viwango sawa vya maendeleo ya binadamu.

Kielelezo la 3:

Mikoa ya Tanzania Bara, kwa mgawanyo wa Alama za ndani za MPI, 2015



Chanzo: Imekokotolewa kwa ajili ya Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu Tanzania 2017 kulingana na matokeo ya utafiti ya TDHS-MIS 2015–16.

Kwa maelezo zaidi, tazama Jedwali na. A5 katika viambatisho vya kitakwimu vya ripoti kuu. ni kwamba, taarifa za umaskini wa kipato kutoka katika tafiti za taifa za matumizi ya kaya kwa Tanzania Bara zinaonyesha kiwango kidogo zaidi cha umaskini kuliko mchanganuo wa Kipimo cha Umaskini kwa vigezo mbalimbali.4 Hesabu ya kipato cha maskini—yaani, uwiano wa watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji muhimu - kwa Tanzania Bara ilikuwa kwenye asilimia 28.8 mwaka 2012, wakati uwiano wa umaskini uliokithiri—yaani, kiwango cha watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa chakula—kilikuwa asilimia 9.7. Hata Hivyo, tofauti za kimikoa bado hazibadiliki. Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha ndiyo mikoa yenye uwiano mdogo wa kaya zinazoishi chini ya mstari wa umaskini wakati mikoa mitatu ambayo ina uwiano mkubwa wa kaya zinazoishi chini ya mstari wa umaskini ni Kigoma, Geita na Kagera (tazama Kielelezo na. 4). Kwa upande wa Zanzibar, umaskini wa mahitaji muhimu umeshuka kutoka asilimia 34.9 mwaka 2009/10 hadi asilimia 30.9 mwaka 2014/15, wakati umaskini uliokithiri ulishuka kwa kiwango kidogo yaani kutoka asilimia 11.7 hadi asilimia 10.8 katika kipindi hichohicho. Udumavu huu wa maendeleo kwa kiasi fulani umesababishwa na ongezeko la bei ya chakula duniani. Kwa kuzingatia kuwa Zanzibar hutegemea chakula chake kutoka nje, ongezeko la bei ya chakula linaweza kusababisha kushuka kwa ustawi visiwani humo.

[4] Taarifa za hesabu za umaskini kwa Tanzania Bara zilipatikana kutoka Utafiti wa Matumizi ya Kaya 2011/12 (NBS 2014); wakati, taarifa kama hizo kwa Zanzibar zilipatikana kutoka Utafiti wa Matumizi ya Kaya kwa Zanzibar 2014-15 (OCGS 2016). Kwa taarifa zaidi, tazama Jedwali na A5 la viambatisho vya kitakwimu katika ripoti kuu.

Kielelezo na. 4:

Hesabu ya uwiano wa kipato cha maskini katika mikoa ya Tanzania Bara, 2012



Chanzo: Makadirio ya Umaskini katika Mikoa na Wilaya ya Tanzania, 2012 (JMT 2015f) uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji muhimu

Matokeo ya Kipimo cha Maendeleo ya jinsia (GDI)5 na Kipimo cha Tofauti ya kijinsia (GII) yanaonyesha kwamba wanawake wana nafasi kubwa zaidi ya kuathiriwa na ukosefu wa maendeleo ya binadamu kutokana na kukosekana kwa usawa baina ya wanawake na wanaume katika elimu, huduma za afya, na fursa za kiuchumi. Alama za GDI kwa Tanzania Bara kwa mwaka 2015 ni 0.864, wakati kwa Zanzibar ni 0.849. Alama hizi zinaashiria kwamba Tanzania inafanya vizuri katika kuziba pengo la jinsia hasa kwa umri wa kuishi na upatikananji wa elimu ya msingi na sekondari. Alama hizi zinaonyesha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kuziba pengo, hasa kuhusu

[5] Kiwango cha msingi kinakaribia 1, kadri kiwango kinavyopungua kutoka kwenye 1 huashiria kupungua kwa pengo kati ya wanawake na wanaume.

makadirio ya umri na upatikanaji wa elimu ya msingi na sekondari. Hata Hivyo, pato la mtu mmoja mmoja kama ilivyopimwa na GDI (kipimo cha pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja), kiwango cha maisha ya wanawake bado kinasuasua kikilinganishwa na kile cha wanaume kwa pande zote, Tanzania Bara na Visiwani.

Kwa kuzingatia Kipimo cha Tofauti ya Kijinsia, Tanzania iliporomoka nafasi nne hadi ya 129 kati ya nchi 188 katika ripoti ya mwisho ya maendeleo ya binadamu duniani (UNDP 2016). Kwa kutenganisha aina na viashiria vilivyotumika kukokotoa Kipimo cha tofauti ya kijinsia, tofauti kidogo ya picha halisi huweza kuonekana. Juhudi zimeendelea kufanywa katika kuongeza uwakilishi wa wanawake bungeni, usawa wa kijinsia katika elimu ya msingi, ongezeko la wanawake katika kazi, na kuongeza umri wa kuishi. Hata Hivyo, tofauti bado imeendelea kuonekana katika uwiano wa wanawake katika nafasi za maamuzi katika ngazi za mikoa na serikali za mitaa, na katika nafasi za uongozi za juu na kati. Wakati huohuo, wanaume wanachukua takriban asilimia 82.6 ya nafasi za uongozi ikilinganishwa na asilimia 17.4 za wanawake. Tofauti ya kijinsia imeendelea kuonekana katika maeneo ya umiliki wa rasilimali mbalimbali, na kwamba, umaskini unaendelea kuwa mzigo mkubwa kwa wanawake wengi wa Kitanzania. Matatizo zaidi hutokana na ongezeko la asilimia ya wanawake wenye umri mdogo ambao wameanza kubeba jukumu la uzazi. Ongezeko hili limekua kutoka asilimia 23 mwaka 2010 hadi asilimia 27 mwaka 2015 (Wizara ya Afya na wengine 2016). Kama ambavyo matokeo haya yanadhihirisha, yafaa kuingilia kati juhudi za kusaidia kukuza usawa wa jinsia na uwezeshwaji wa wanawake ili kulinda haki za msingi za wanawake na kuhamasisha uwezeshaji wa wanawake katika kuchangia mageuzi ya kijamii na kiuchumi.

Vichocheo vya Maendeleo ya Binadamu Nchini Tanzania: Matokeo ya Utafiti kuhusu Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu na Kipimo cha Umaskini kwa vigezo mbali mbali

Ili kuainisha mambo muhimu yanayosababisha maendeleo ya binadamu nchini Tanzania, Kipimo cha maendeleo ya binadamu na kipimo cha umaskini kwa kutumia vigezo mbali mbali vilichanganuliwa. Ufuatao ni muhtasari wa matokeo ya utafiti huo.

Kipato

Kipimo kilichotumika kupima viwango vya maisha ya watu (living standards) katika HDI ni kipato. Ili kuweza kukadiria tofauti za vipato kwa nchi na nchi, UNDP hutumia Pato la Jumla la Taifa (GNI) kwa mtu mmoja mmoja. Hata Hivyo, kutokana na vikwazo katika matokeo ya tafiti za taifa, ripoti ya THDR 2017 hutumia Pato la Ndani kwa mtu mmoja mmoja.6

Pato la Ndani kwa mtu mmoja mmoja kwa Tanzania Bara limekuwa likiongezeka katika muongo uliopita hadi kufikia shilingi 1,918,929/= mwaka 2015, kutoka shilingi 1,025,038 mwaka 2012. Viwango vya mapato vimetofautiana sana, ambapo kiwango cha juu kilikuwa shilingi 3,035,543 kwa mtu mmoja mmoja kwa mkoa wa Dar es Salaam na kile cha chini kilikuwa shilingi 1,075,268 kwa mtu mmoja mmoja mkoani Kagera (JMT 2016b).

Kielelezo na. 5 kinaonyesha mwelekeo na Malengo ya muda mrefu kwa kipato cha mtu mmoja mmoja kwa dola za Marekani. Mwaka 2014 Tanzania ilifikia Pato la Ndani la kiasi cha dola za Marekani 1,043 kwa mtu mmoja mmoja. Lengo likiwa ni kufikia dola za Marekani 3,000 ili kufikia lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo ya kuwa nchi ya kipato cha kati kufikia mwaka 2025.

[6] Pato Ghafi la Taifa ni jumla ya thamani ya kiuchumi iliyozalishwa na wazalishaji wa ndani. Inawakilisha thamani ya fedha kwa bidhaa na huduma zote zilizozalishwa katika kipindi maalum, mara nyingi huwa ni mwaka mmoja, kabla ya kuingizwa katika matumizi ya mitaji isiyohamishika. Ni jambo la kawaida kufafanua Pato Ghafi la Taifa kwa kuzingatia kipato cha mtu mmoja mmoja. Pato Ghafi la Taifa mtu mmoja mmoja hupatikana kwa kugawanya Pato la Ghafi la Taifa kwa jumla ya idadi ya watu kwa mwaka husika. Huonesha kiasi ambacho kila mtu katika nchi angeweza kupata ikiwa Pato Ghafi la Taifa lingegawanywa sawasawa.

Kielelezo na. 5:

Mwelekeo na Malengo ya Pato la Mtu Mmoja Mmoja, 2007 hadi 2025



Source: FYDP II (URT 2016a)

Afya

Kwa kipindi cha mwaka 2002 hadi 2012, umri wa kuishi uliongezeka kwa takriban miaka 9 kwa wanaume (kutoka miaka 51 hadi miaka 60), na takriban miaka 13 kwa wanawake (kutoka miaka 51 hadi miaka 64) (tazama Jedwali na. 1). Wastani wa umri wa kuishi kwa Tanzania Bara ni miaka 61.7 na miaka 65.7 kwa Zanzibar. Ongezeko hili limechangiwa na uboreshaji wa masuala mbalimbali, ikiwemo kupungua kwa vifo vya watoto, kupungua kwa vifo vitokanavyo na VVU/UKIMWI, maboresho ya lishe na usafi, ongezeko la upatikanaji wa maji safi ya kunywa, uzazi wa mpango pamoja na utoaji wa chanjo.

Jedwali na. 1:

Matarajio ya umri wa kuishi toka kuzaliwa nchini Tanzania, 2002 na 2012

Hata Hivyo, licha ya maboresho ya wazi katika kudhibiti na kupunguza wagonjwa, bado malaria inaonekana kuwa

	Umri wa kuishi toka kuzaliwa, 2002			Umri wa kuishi toka kuzaliwa, 2012		
	Jumla	Wanaume	Wanawake	Jumla	Wanaume	Wanawake
Tanzania	50.9	51.0	51.0	61.8	59.8	63.8
- Rural	50.0	49.9	50.4	62.4	60.3	64.4
- Urban	56.8	55.8	58.8	59.7	57.7	61.7
Tanzania Bara	50.4	50.8	51.0	61.7	59.7	63.7
- Rural	49.4	49.4	51.2	62.6	60.6	64.6
- Urban	56.4	55.5	58.8	59.9	58.0	61.8
Zanzibar	59.0	59.7	60.3	65.2	63.3	67.1
- Rural	58.7	58.0	59.9	65.5	64.0	66.9
- Urban	56.8	55.5	57.8	64.9	62.2	67.6

Source: URT 2015a

ni chanzo kikuu cha maradhi na vifo. Watoto chini ya umri wa miaka mitano wanaonekana kuwa katika mazingira hatarishi zaidi, wakifuatiwa na wanawake wajawazito ambao wana uwezekano wa kupata maambukizi ya malaria mara nne zaidi ya wanawake ambao si wajawazito. Ingawa Tanzania imeweza kudhibiti maambukizi ya VVU/UKIMWI, bado yanachangia kushuka kwa umri wa kuishi. Tafiti za mwaka 2007-08 na 2011-12 za Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria (THMIS) zinaonyesha kwamba maambukizi ya VVU yamepungua kwa kiasi kidogo kutoka asilimia 5.7 hadi 5.1 miongoni mwa watu wazima wenye umri kati ya miaka 15-49 (TACAIDS et al. 2008, 2013). Kijinsia, maambukizi kwa wanawake ni asilimia 6.2 wakati kwa wanaume ni asilimia 3.8.

Vifo vya utotoni, ambavyo ni kiashiria kimojawapo kati ya viashiria vikuu vya masuala ya afya katika Kipimo cha umaskini kwa vigezo mbali mbali (MPI), vimeshuka katika kipindi cha miaka 25 iliyopita. Kwa mfano, kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka mitano (U5MR) kimeshuka kutoka vifo 141 katika kila vizazi hai 1,000 mwaka 1990 hadi vifo 67 mwaka 2015-16 (tazama Kielelezo na. 6). Kushuka huku kumetokana na maboresho endelevu katika sekta ya afya, hasa katika afya ya uzazi na watoto; na kipekee, ni maboresho kwenye utoaji wa chanjo na juhudi za kuzuia malaria. Hata Hivyo, pamoja na maboresho hayo katika kuzuia na kupunguza magonjwa, bado malaria inaendelea kuwa ni chanzo kikuu cha maradhi na vifo.

Kielelezo na. 6:

Mwelekeo wa Vifo vya Watoto Tanzania, vifo vya watoto chini ya miaka mitano na vichanga, 1990 hadi 2016



Chanzo: Imekokotelwa kwa ajili ya THDR 2017 kwa kuzingatia taarifa za DHS kutoka miaka tofauti

Kadhalika, licha ya maboresho hayo, lishe duni miongoni mwa watoto wa Tanzania bado ni jambo zito na linalojitokeza sehemu nyingi. Utafiti wa TDHS-MIS (2015–16) ulibaini kuwa asilimia 34 ya watoto walio chini ya miaka mitano walikuwa wamedumaa, asilimia 14 walikuwa na uzito pungufu au wembamba sana wakilinganishwa na umri wao, na asilimia 5 walikuwa wamedhoofika au wembamba sana wakilinganishwa na vimo vyao. Zaidi ya hayo, tangu 1999 na 2016 bado hakuna mabadiliko yoyote katika viwango vya udumavu ambayo ni dalili ya utapiamlo uliokithiri. Taarifa zinaonyesha pia tofauti za msingi katika hali ya lishe kwa kuzingatia kipato cha kaya na mikoa. Kwa mfano, kiwango cha udumavu miongoni mwa watoto wadogo kilitofautiana kutoka asilimia 15 katika mkoa wa Dar es Salaam hadi asilimia 49 katika mkoa wa Njombe. Na, hatari ya kuwa na utapiamlo uliokithiri kwa watoto wanaotoka katika kaya maskini ni kubwa mara tatu zaidi kuliko watoto wanaotoka katika kaya zenye unafuu wa maisha. Viwango hivyo vya juu vya kukithiri kwa lishe duni havisababishwi tu na umaskini na ukosefu wa chakula, bali pia husababishwa na matatizo ya malezi ya vichanga na watoto wadogo pamoja na namna ya kuwalisha katika ngazi ya kaya.

Maendeleo ya Elimu na Ujuzi

Elimu ni kichocheo kimojawapo cha maendeleo ya binadamu, na ni kipimo muhimu cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) na Umaskini kwa kutumia kipimo kwa vigezo mbali mbali (MPI). Elimu ni suala muhimu katika kujenga uwezo wa jumla wa binadamu pamoja na kuendeleza ujuzi na maarifa ya kiteknolojia kwa wafanyakazi, ambao ni muhimu kwa mageuzi ya kiuchumi. Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, miaka inayotarajiwa kutumika kwa kusoma (EYS) kwa mtoto wa Tanzania Bara ilikuwa 8.9, na kwa mtoto wa Zanzibar ilikuwa 10.8 (JMT 2015c). Kadhalika, sensa hiyo ilionyesha pia tofauti ya miaka ya kuwa masomoni (EYS) kwa watoto katika mikoa ya Tanzania Bara. Miaka ya kuwa masomoni kwa watoto mkoani Tabora ni miaka 6.2, ambayo ni pungufu ya miaka 5 ya EYS ya mtoto katika mkoa wa Kilimanjaro (yaani, miaka 11.4).

Taarifa za utafiti wa THDS-MIS 2015-16 inaonyesha kuwa asilimia ya watu wasio na elimu rasmi imekuwa ikipungua. Mwaka 2015, takribani asilimia 24 ya wanawake na asilimia 19 ya wanaume hawakuwa na elimu rasmi. Hata hivyo, kiwango cha kuhitimu shule, kiliendelea kuwa chini sana; takribani theluthi ya idadi ya watu nchini Tanzania wamehitimu elimu ya msingi, lakini waliohitimu elimu ya sekondari ni pungufu ya moja ya kumi. Kwa hakika, watoto wa mijini wanawazidi mara nne au tano watoto wa vijijini katika nafasi ya kuhitimu elimu ya sekondari (MoHCDGEC na Wenzake. 2016). Viwango vya kufeli mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi bado vimebakia vilevile; ni asilimia 67.8 tu ya wanafunzi wa Tanzania Bara waliofanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka 2015 ndio walifaulu. Taarifa hizi zinaonyesha wazi kuwa vijana wengi ama hawahitimu elimu ya msingi au wanakamilisha elimu ya msingi bila kupata maarifa na ujuzi kwa kiwango kilichomo katika mtaala wa elimu ya msingi.

Bado kuna matatizo pia katika elimu ya sekondari. Uwiano wa kuandikisha wanafunzi katika shule za sekondari za chini (Kidato cha I hadi cha IV) umepungua kutoka asilimia 37.6 mwaka 2012 hadi asilimia 33.4 mwaka 2016. Kwa hakika, wanafunzi wa maeneo ya mijini wana nafasi kubwa zaidi ya kusoma elimu ya sekondari, wakiwazidi wenzao wa vijijini zaidi ya mara mbili. Na, wanafunzi wanaotoka katika kaya tajiri wanawazidi takribani mara nane wale watokao katika kaya maskini katika kusoma elimu ya sekondari.

Licha ya kufanikisha upatikanaji wa elimu bora katika ngazi ya msingi na sekondari, ukuzaji wa uwezo wa binadamu kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi unahitaji uwekezaji katika mafunzo ya ujuzi. Kwa mfano, utafiti uliofanywa mwaka 2014 kuhusu nguvukazi uliripoti kuwapo kwa kiwango cha chini cha ujuzi wa kawaida, ambao huathiri uzalishaji (URT 2016f). Tafiti pia zinajaribu kuonyesha msigano baina ya ugavi na mahitaji ya maarifa. Hii inahusisha aina na hadhi ya maarifa ambayo wahitimu wanapata katika taasisi za ufundi stadi, vyuo vya ufundi, pamoja na vyuo vikuu. Kwa mfano, karibu asilimia 80 ya nafasi za kazi zilizopo, zikiwemo zitakazohitajika kwa miaka mitatu mpaka mitano ijayo, ni zile za sayansi na hesabu. Hata hivyo, haya ni masomo ambayo yana viwango vidogo vya ufaulu katika mitihani ya kidato cha IV na VI. Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuziba baadhi ya mapengo haya ya maarifa, na kwamba, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano II wenyewe unasisitiza umuhimu wa kuboresha mafunzo rasmi ya maarifa katika sekta za kipaumbele.

Ubora wa Maisha

Kipimo cha Umaskini kwa vigezo mbali mbali huangalia viashiria sita vya hali za kaya ili kupima maisha bora ya watu navyo ni: upatikanaji wa maji safi na salama, upatikanaji wa vifaa vya usafi, umiliki wa rasilimali, aina ya nishati ya kupikia inayotumika, upatikanaji wa umeme, na aina ya sakafu katika makazi. Mwelekeo wa hivi karibuni kuhusiana na viashiria hivi unatoa matumaini, ila bado kuna mengi yanahitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha hali ya maisha ya Watanzania walio wengi. Mathalani, asilimia ya kaya zenye uwezo wa kufikia vyanzo bora vya maji ya kunywa imeongezeka kutoka 54 mwaka 2010 hadi asilimia 61 mwaka 2015-16 (MoHCDGEC et al. 2016, NBS na ICF Macro, 2011). Hata hivyo, kwa kuangalia makazi, ni nusu tu ya kaya za vijiji kwa Tanzania Bara, ambayo ni sawa na asilimia 49, zina uwezo wa kufikia vyanzo bora vya maji ikilinganishwa na asilimia 86 ya kaya za mijini na asilimia 98 za Zanzibar.

Uwiano wa kaya zenye uwezo wa kupata huduma ya choo inayokubalika ni mdogo, na unapungua (tazama Kielelezo na. 7). Kwa ujumla, asilimia 55 ya kaya zinatumia vyoo duni na asilimia 10 ya kaya hazina vyoo kabisa.

Kielelezo na 7:

Huduma ya choo kwenye kaya (% ya kaya)



Chanzo: MoHCDGEC et al. (2016, 23)

Umiliki wa rasilimali zinazodumu, kama vile redio, jokofu, na simu (za mkononi) ni kiashiria cha wazi kinachoonesha hali ya kijamii na kiuchumi ya kaya. Tafiti za 2015–16 TDHS-MIS ziligundua kwamba karibu kaya 8 kati ya 10 (sawa na asilimia 78) zinamiliki simu za mkononi; karibu nusu ya kaya zote (sawa na asilimia 52) zinamiliki redio; kaya moja kati ya tano (sawa na asilimia 20) inamiliki televisheni; na ni asilimia 9 tu ya kaya zote ndo inamiliki jokofu. Kwa kuangazia tofauti nyingine za kijografia, umiliki wa rasilimali katika kaya uko juu miongoni mwa kaya za mijini kwa Tanzania Bara na Zanzibar kuliko zile za vijijini kwa Tanzania Bara.

Kigezo kingine kinachoathiri hali za maisha za Watanzania ni aina ya nishati inayotumiwa na kaya husika. Kupikia kwa nishati ngumu—kama mkaa, kuni, mabua, vijiti, na nyasi—huweza kusababisha moshi ndani ya nyumba na visababishi vingine vyenye hatari ya kuharibu afya za wakazi. Ripoti ya 2015–16 TDHS-MIS ilibaini kuwa zaidi ya kaya 9 kati ya 10 (sawa na asilimia 94) nchini Tanzania zinatumia nishati ngumu kwa kupikia, hasa kuni (kwa asilimia 66) na mkaa (kwa asilimia 27). Matokeo yanaonyesha zaidi kwamba, kwa miaka mitano iliyopita, matumizi ya kuni yamepungua, lakini matumizi ya mkaa yameongezeka. Kitaifa, karibu robo ya kaya (sawa na asilimia 23) zina umeme. Pia, pengo kati ya miji na vijiji ni kubwa; asilimia 56 ya kaya za mijini zina umeme ikilinganishwa na asilimia 5 ya kaya za vijijini kwa Tanzania Bara. Karibu kila kaya moja kati ya mbili visiwani Zanzibar zina umeme. Hii ni sawa na asilimia 47.

Mabadiliko ya idadi ya watu na maendeleo ya binadamu nchini Tanzania

Ripoti pia inaweka bayana changamoto kubwa za maendeleo zinazosababishwa na ongezeko kubwa la watu na ukuaji wa miji. Katika miaka 35 iliyopita, idadi ya watu katika nchi imeongezeka karibu mara tatu na kufikia watu milioni 50.1 (makadirio ya mwaka 2016). Wastani wa ongezeko la kiwango cha asilimia 2.7 kwa mwaka unaonekana kuwa mojawapo ya wastani mkubwa duniani; na hii inamaanisha ongezeko la watu milioni 1.2 kila mwaka (Otieno, Amani na Makbel 2016). Kwa kiwango cha sasa, idadi ya watu nchini Tanzania inaelekea kufikia milioni 67 ifikapo mwaka 2025 na baadaye milioni 89.2 ifikapo mwaka 2035 (tazama kielelezo na. 8).

Kielelezo na. 8:

Idadi ya watu nchini Tanzania (1948–2035)



Chanzo: Data kutoka sensa ya taifa kwa mwaka 1948 hadi 2012. Tafiti kwa 2015 na baadaye makadirio kutoka NBS kwa kuzingatia mwendelezo kutoka idadi ya watu na sensa ya makazi ya mwaka 2012.

Kwa kuangazia data kutoka TDHS-MIS 2015-16, kielelezo na. 9 kinaonyesha mgawanyo wa idadi ya watu nchini Tanzania kwa mgawanyo wa umri wa miaka-mitano, unaotofautishwa na jinsia. Kitako kikubwa cha piramidi kinafafanua kuwa sehemu kubwa ya watu nchini Tanzania ni wenye umri, kitu ambacho ni mfano halisi wa nchi zenye wastani mdogo wa umri wa kuishi pamoja na kiwango kikubwa cha vifo. Karibu nusu ya jumla ya idadi ya watu iko chini ya miaka 17.5. Muundo wa idadi ya watu nchini Tanzania kwa kigezo cha uwiano wa umri-jinsi umebaki hivyo bila kubadilika kwa muongo uliopita.

Kielezo na. 9:

Mgawanyo wa idadi ya watu katika kaya nchini Tanzania kwa Umri-jinsi, 2012



Chanzo: MoHCDGEC et al. (2016, 25)

Age= umri | Male =Wanaume | Female =wanawake

Ongezeko kubwa la watu na ukuaji wa miji vimesababisha changamoto kubwa kwa uwezo wa serikali kukidhi mahitaji ya miundombinu ya umma na vifaa, makazi, ajira, na huduma za jamii, hususani elimu, afya, na maji. Kwa mfano, ripoti ya Utafiti wa Nguvukazi ya mwaka 2014 inaeleza kwamba, kati ya mwaka 2006 na 2014, umri wa watu walio katika kipindi cha kufanya kazi (yaani, miaka 15 na kuendelea) ulipanda kwa watu milioni 4.8 hadi kufikia milioni 25.8, ongezeko kubwa likiwa katika maeneo ya mijini. Ongezeko hili kubwa la nguvu kazi linamaana kubwa katika masuala ya sera za kutengeneza ajira na ukuzaji wa maarifa, hususani ikizingatiwa kwamba vijana ni asilimia 55 ya nguvu kazi nchini. Ili kupunguza idadi ya watu wanaoingia katika kundi la watafuta kazi kila mwaka, juhudi za serikali zitahitajika ili kupunguza kiwango cha ongezeko la watu kwa kuhusisha na mikakati ya kiuchumi ili kupata ajira zinazofaa.

2.

Dhima ya sera ya kijamii katika mageuzi ya kiuchumi

Kama ilivyoelezwa katika utangulizi, maudhui ya sura tatu za ripoti ya mwaka huu zinafafanua dhima na nafasi ya sera ya kijamii katika mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea nchini Tanzania. Sura hii inabainisha nadharia inayoelezea uhusiano kati ya sera ya kijamii na kiuchumi kuelekea katika mageuzi ya kiuchumi sambamba na maendeleo ya binadamu. Hoja ya msingi ya sura hii ni kwamba, sera ya kijamii lazima iwiane na Malengo ya mageuzi ya kiuchumi sambamba na matokeo ya kijamii yanayotamaniwa.

Kwa fasili pana, sera ya kijamii hujumuisha vipengele mbalimbali vya sera ambavyo huathiri namna watu wanavyoishi kupitia juhudi za pamoja au za kibinafsi. Sera ya kijamii hufafanua Malengo yanayopishana katika kutoa ulinzi, usambazaji wa mali na kipato, pamoja na kuwezesha uzalishaji wa kijamii pamoja na utoaji huduma. Ufanisi wa kiuchumi na uzalishaji huathiriwa moja kwa moja na Malengo haya ya kisera. Sera ya kijamii ina athari zisizo za moja kwa moja ambazo mara nyingi hazionwi. Athari hizo ni pamoja na: Kuchochea njia mpya za uvumbuzi; kupunguza hatari na mashaka katika uwekezaji wa karibu; kutoa rasilimali fedha kwa ajili ya uwekezaji na athari ya kuboresha utengenezaji wa mtaji wa watu kwa kuwekeza katika afya na elimu.

Tuchukulie mfano mmoja wa kupanua hifadhi ya kijamii kupitia mifumo ya uchangiaji (kwa mfano, mifuko ya pensheni) au mifumo isiyo ya uchangiaji (kama vile ulipaji wa fedha taslimu) ni njia ya moja kwa moja ya kupunguza umaskini na utengwaji. Hata Hivyo, pamoja na faida za moja kwa moja, mifumo hii inaweza kuchochea mageuzi ya kiuchumi kwa namna mbalimbali muhimu: Kwanza, vipengele vya hifadhi vya sera ya kijamii—ambavyo huruhusu kaya kubainisha mahitaji yao ya msingi—pia kuchochea unyumbufu wa kaya kwa kuboresha kipato halisi pamoja na viwango vya elimu, kwa kuruhusu familia maskini kupeleka watoto wao shuleni. Pili, katika ngazi ya kaya na ya mtu binafsi, hifadhi ya kijamii huweza kuondoa hatari na kuboresha uwekezaji katika shughuli mpya na zenye uzalishaji zaidi wa kiuchumi. Tatu, kipato cha ziada cha kaya huongeza pia mahitaji, hivyo, kuchochea maendeleo ya uchumi wa taifa. Mwisho, mifumo ya uchangiaji wa hifadhi ya kijamii, kama vile, mifuko ya pensheni, huweza kubeba—na kihistoria ulimwenguni kote imeweza kubeba—dhima ya mageuzi kwa kutoa rasilimali fedha kwa ajili ya uwekezaji wa ndani, kama vile maendeleo ya vifaa vya viwanda. Kwa mfano, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) unafadhili kiwanda kiitwacho Agave Syrup Factory kilichopo Tanga kama juhudi za kuboresha viwanda vya ndani vya dawa za binadamu. Kupanuliwa kwa mifumo ya uchangiaji huweza pia kuchangia ukuaji wa sekta ya fedha, hii itamaanisha kuongezeka kwa usambazaji wa mitaji ya muda mrefu pamoja na kupunguza gharama za mtaji. Kielelezo namba 10 kinaonyesha vipengele vya msingi vya hifadhi za kijamii nchini Tanzania.

Kielelezo namba 10:

Vipengele vya msingi vya hifadhi za jamii nchini Tanzania



Chanzo: Myamba na Kaniki (2016, 7)

Usambazaji wa faida za ukuaji—ambazo hupatikana kupitia sera za fedha zinazopambanua kodi na matumizi—huweza pia kuwa na athari za wazi kwenye umaskini kwa kuinua vipato vya maskini na kuleta matokeo chanya katika maendeleo ya kiuchumi. Usambazaji, kwa umahsusi wake, huweza kusaidia kupambanua ongezeko la kutokuwapo kwa usawa kama ukuaji wa kiuchumi. Hili ni jambo muhimu kwa sababu kutokuwapo kwa usawa huweza kuathiri ukuaji wa viwanda kwa kupunguza mahitaji ya jumla, kuongeza ghasia za kisiasa, na kuingiza gharama za muda mrefu za sera ya kijamii. Nchini Tanzania, pengo la kipato cha mtu binafsi na cha kaya limekuwa likiongezeka tangu katikati ya miaka ya 1990. Hali hii inaashiria uhitaji wa kufikiri upya uhusiano kati ya usambazaji na ujenzi wa viwanda, hivyo kutengeneza mazingira bora zaidi kwa mageuzi endelevu ya kiuchumi.

Mbali na uwekezaji katika vitega uchumi kama vile majengo na viwanda, maendeleo ya mtaji wa binadamu ni kipengele muhimu cha mageuzi ya viwanda na muundo wa uchumi. Mageuzi ya teknolojia ya uzalishaji yako katika kiini cha kufanikisha uanzishaji wa viwanda, na matumizi ya teknolojia mpya huhitaji uwezo wa kiteknolojia. Haishangazi kuona kwamba nchi zilizoendelea (kwa kasi) kiviwanda zimewekeza sana katika mifumo ya elimu, huku zikilenga kwenye elimu ya ufundi na utaalamu ili kusukuma mbele lengo la kupanua viwanda. Uwekezaji wa jamii kwenye elimu na afya, pamoja na sera nyingine za kijamii zinazoelezea hifadhi, uzalishaji na usambazaji wa kijamii, huchangia katika kuendeleza uwezo wa ujuzi na teknolojia kwa wafanyakazi. Hivyo, sera ya kijamii ina dhima katika kuboresha uvumbuzi, upanuzi na usambazaji wa uwezo wa kiteknolojia kwa ajili ya kuliweka wazo la uanzishaji wa viwanda katika uhalisi. Mpango wa Miaka Mitano II hutoa wito wa kuendeleza uwezo wa wafanyakazi ambao ni msingi wa uanzishwaji wa viwanda. Hata Hivyo, sera ambazo zinalenga kwenye maendeleo ya ujuzi ili kuboresha mtaji wa binadamu huhitaji kuzingatia hali halisi ya mwenendo wa wafanyakazi pamoja na mabadiliko ya idadi ya watu kama hoja ya msingi.

Ukiachilia mbali athari zake kwenye mambo yanayohusiana na ugavi, sera za kijamii zina dhima muhimu lakini husahauliwa mara nyingi katika uga wa uchumi. Suala la kuwapo kwa mahitaji lina maana sana katika uanzishwaji wa viwanda. Kwa mfano, uanzishwaji wa viwanda unaweza kuwa na athari za msingi kwenye mwelekeo wa mahitaji katika uchumi uliopo. Zaidi, huweza kutokea kwa gharama za viwango vya maisha ya maskini. Ukuaji kupitia uanzishwaji wa viwanda husababisha kuongezeka kwa mahitaji muhimu, hasa chakula. Sekta ya kilimo inaposhindwa kubadilika ili kusambaza ongezeko hili la mahitaji, na ongezeko la uagizaji wa bidhaa za msingi

huongeza kutokuwapo kwa uwiano wa kibiashara, mahitaji huzidi usambazaji kiasi cha kusababisha mfumuko wa bei kwa bidhaa muhimu. Ijapokuwa hali hii huathiri maisha ya watu wote, huwaathiri zaidi watu maskini, ikizingatiwa kuwa asilimia kubwa ya kipato chao hutumika katika bidhaa za lazima. Kwa hiyo, sera ya kijamii lazima zitazamwe kama nyenzo ya lazima ya kusahihisha mpishano huu, kuliko kuwa kama kitu kinachoidhuru hali ya sasa kiasi cha kuzuia ukuaji wa muda mrefu.

Sera ya kijamii huweza pia kubeba dhima muhimu ya kufafanua mahitaji kupitia rasilimali za mahitaji ya msingi. Katika kipindi cha baada tu ya uhuru, wakati wa Mkakati wa Viwanda (Basic Industry Strategy), malengo ya kijamii yaliwekwa bayana na kuhusishwa na aina ya viwanda vilivyohitajika ili kuyatimiza. Kwa mfano, utoaji wa huduma za afya huhitaji bidhaa na huduma kama vipengele muhimu vya uzalishaji, ikihusisha madawa, ruzuku ya madawa na vifaa-tiba, pamoja na ruzuku ya vitu vingine kama vile vifungashio na vifaa vya usafi. Hivyo, kutumia mifuko ya umma kwa ajili ya ugawaji wa huduma za afya huweza kuboresha uanzishwaji wa viwanda kwa kutoa fursa kwa uwekezaji wa viwanda na biashara ndani ya uchumi wa ndani. Hii huonyesha zaidi ni namna sera ya kijamii na mageuzi ya kiuchumi vyaweza kwenda sambamba.

Kwa hiyo, sera za kijamii zinaweza kubadilishwa kwa namna mbalimbali pale zinapobeba dhima ya kurekebisha aina ya shughuli za kiuchumi, kasi na aina ya uvumbuzi, na mwelekeo wa ulaji unaokuwepo kadiri ukuaji unavyojitokeza. Zaidi ya hayo, sera za kiuchumi—na siyo sera ya kijamii kama zinavyotafsiriwa kwa namna rahisi—huweza kuwa na athari muhimu katika matokeo ya kijamii. Hii humaanisha kuwa sera za kiuchumi na za kijamii kwa asili hujengana; sera ya kijamii zina viashiria vya kiuchumi vyenye wigo mpana, na sera za kiuchumi zitabeba dhima ya msingi na ya moja kwa moja katika kuleta matokeo ya kijamii. Hivyo, muingiliano wa sera za kiuchumi na za kijamii unahitajika kuiongoza Tanzania kwenye njia ya maendeleo ambako mahitaji ya binadamu yatatimizwa kwa wakati.

3.

Kufungamanisha sera za kiuchumi na za kijamii - msisitizo unaobadilika katika mwongozo wa sera ya taifa tangu uhuru

Sura ya tatu inatoa mtazamo wa kihistoria kuhusu kufungamana kwa sera za kiuchumi na za kijamii katika suala zima la sera za Tanzania tangu nchi ipate uhuru. Inaonyesha kuwa kufungamana kwa sera ya kijamii na kiuchumi siyo jambo jipya nchini Tanzania, lakini asili na kiasi cha mwingiliano huo kimetofautiana kulingana na mabadiliko ya sera katika awamu mbalimbali. Mafunzo kutokana na uzoefu wa huko nyuma yalipatikana kwa kuchanganua mfungamano wa sera za kiuchumi na za kijamii katika vipindi vinne: 1) Tangu uhuru hadi Azimio la Arusha (1961-66); 2) Tangu Azimio la Arusha hadi mdororo wa kiuchumi (1967-1985); 3) Kipindi cha mipango ya urekebishaji wa uchumi kuanzia 1986 hadi 1996; na 4) Kipindi cha kuanzia 1996 hadi 2016 wakati serikali ya Tanzania ikijitahidi upya kudhibiti ajenda ya maendeleo ya taifa.

Uhuru hadi Azimio la Arusha (1961-66)

Kufuatia kupatikana kwa uhuru mnamo mwaka 1961, serikali ya Tanganyika ilijikita katika mpango wa kuhakikisha kwamba sekta ya umma inapewa sura ya kiafrika zaidi sambamba na juhudi za makusudi za kuinua uchumi. Muundo wa uchumi kwa maana ya mahusiano ya kiuzalishaji, umuliki wa mali, na vipaumbele vya mazao ulikuwa bado unalenga soko la nchi zilizoendelea kwa viwanda uliopendelea zaidi bidhaa za anasa pamoja na usafirishaji wa mali ghafi au uchakataji wa awali wa bidhaa kwa ajili ya kuzisafirisha nje. Zaidi ya hayo, ukoloni ulichochea mgawanyo wa jamiii kwa misingi ya rangi na kiuchumi. Muundo wa sera iliyokuwapo ulisisitiza maendeleo ya sekta binafsi, na uchumi uliegemea sana katika sekta binafsi zilizomilikiwa na wageni, vitega uchumi vya nje, na misaada. Kimsingi, Serikali haikuhoji masuala ya msingi kuhusiana na kutokuwapo kwa usawa katika mgawanyo wa kipato na mali katika jamii au mgawanyo wa kazi kwa misingi ya rangi au kuhusu mpishano katika muundo wa uchumi.

Kinyume chake, vipaumbele vilielekezwa kwenye mageuzi ya kilimo kwa kutumia mbinu za kisasa za kilimo ili kuongeza uzalishaji. Njia hii ilihusisha uhamishaji wa baadhi ya wakulima kutoka vijiji vyao vya asili kwenda katika vijiji au makazi mapya ili kuharakisha uanzishwaji wa mageuzi ya kijamii na kiuchumi. Hii ilifanyika kwa kufikiri kuwa wakulima wadogowadogo walikuwa maskini kwa sababu walikosa mtaji pamoja na teknolojia. Hata hivyo, njia hii ilishuhudia kushindwa kwa kiasi kikubwa, kuundwa kwa kundi lililonufaika zaidi, kuongezeka kwa tofauti za kijamii pamoja na matokeo duni ya kiuchumi kutokana na gharama kubwa na zisizohimilika. Ilidhihirika wazi zaidi kuwa mabadiliko ya kimuundo na mageuzi ya kiuchumi yalikuwa lazima yabadili muundo wa kiuchumi na kijamii ulioharibiwa. Mambo haya yalikuwa ya muhimu kuzingatiwa wakati wa kutungwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967.

Azimio la Arusha hadi mdororo wa kiuchumi (1967-1985)

Azimio la Arusha lilisababisha mabadiliko ya itikadi na kutangaza misingi ya Ujamaa na Kujitegemea ili kufafanua hali iliyokuwepo kwa ajili ya maendeleo baada ya uhuru (TANU 1967). Dhana muhimu iliyohifadhiwa katika Azimio la Arusha ilikuwa ni maendeleo ya watu. Azimio lilifafanuliwa kwa upana ikiwa ni pamoja ukombozi wa kijamii na wa kiuchumi huku likijikita katika hadhi ya binadamu, usawa na uhuru wa kila mmoja, fursa sawa kwa watu wa rangi zote, kuwa na msimamo wa kupunguza tofauti za kipato na utajiri, pamoja na kupambana na rushwa. Katika kipindi hiki chini ya uongozi wa Rais Nyerere, masuala ya kijamii yalikuwa lazima yashughulikiwe na sera za Serikali kuhusu mageuzi ya uchumi na viwanda.

Msimamo wa kutunga sera katika miaka ya mwishoni mwa 1960 na 1970 ulisisitiza umiliki wa pamoja wa njia kuu za uzalishaji mali kupitia utaifishaji na upanuzi wa taasisi za umma. Kwa mageuzi ya kilimo na vijiji, mbinu mpya iliyochaguliwa ni ile ya uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa (ujamaa kwa Kiswahili hufasiliwa kama 'udugu wa kifamilia'). Hivyo, dhana hii iliwezesha uanzishwaji wa vijiji kupitia shughuli za hiyari na za kujitegemea za watu

wenyewe. Ujamaa ulikuwa na Malengo mawili ya kiuchumi na kijamii: Kuwa na uchumi unajitosheleza na kupata maendeleo ya kijamii kama jamii za vijijini.

Hata hivyo, kinyume na msisitizo aliouweka Nyerere katika ushauri na uhusishwaji wa watu, mpango wa ujamaa vijijini ulidhoofishwa kwa kukosekana ushauri kutoka kwa wanavijiji kuhusu mpango wenyewe na manufaa yake, matokeo yake njia zisizo za kidemokrasia na rasmi zilitumika kulazimisha utekelezaji wa mpango huo. Hata Hivyo, matokeo ya mpango wa vijiji vya ujamaa kama msingi wa kujenga uchumi wa kiwango hayakufanikiwa. Mashamba ya ushirika hayakuzalisha kama ilivyofikiriwa. Kwa hakika, uzalishaji katika mashamba chini ya mpango wa vijiji vya ujamaa ulikuwa mdogo kuliko ule uliokuwa unapatikana katika mashamba ya wakulima binafsi katika miaka ya 1970.

Mkakati wa Viwanda vya Msingi (Basic Industry Strategy - BIS) ulioanzishwa mwaka 1975 pia ulilenga kupata mabadiliko ya kimuundo na kujitegemea. Kwa kiasi kikubwa, uzalishaji wa viwanda ulitaifishwa, na mkazo uliwekwa katika viwanda vilivyozalisha bidhaa za kukidhi mahitaji ya ndani, hususani mahitaji muhimu ya watu, yakijumuisha huduma za jamii kama afya, elimu na makazi, wakati huohuo zikitolewa bidhaa za kukuza mtaji wa uchumi. Kwa hiyo, viwanda vilivyopewa kipaumbele kupitia Mkakati wa Viwanda ni vya nguo, viatu, dawa, karatasi, na vifaa vingine vya elimu. Sera ya afya ambayo ililazimisha kutolewa kwa huduma bure za afya kwa wananchi wote ilihusishwa na sera ya viwanda. Maendeleo ya viwanda yalihusisha mahitaji ya sekta ya afya kama vile dawa na ruzuku za mambo mengine. Katika elimu, sera ya Elimu ya Kujitegemea (EK) ya mwaka 1967 pia ilibeba dhima mbili: Kuwezesha upatikanaji wa maarifa na ujuzi kwa ajili ya kubainisha changamoto za jamii au kutimiza mahitaji ya soko la ajira, na wakati huohuo kufundisha amali za kijamii ambazo ni msingi wa kujenga taifa (Nyerere, 1968).

Nafasi ya mahitaji na matumizi katika kuboresha matokeo ya kiuchumi nchini Tanzania haikutekelezwa vema kwa hoja kwamba vikwazo vya msingi vilivyokuwa vinaikumba Tanzania vilitokana na suala la uzalishaji bidhaa. Mkazo uliowekwa kwenye uwekezaji ulizidi wa matumizi ya kawaida ambao ungehakikisha matumizi sahihi ya uwezo uliokuwa umezalishwa. Uwekezaji wa viwanda ulizidishwa mara nne kati ya mwaka 1968 na 1979. Jambo hili lilileta matokeo ya wazi katika maendeleo ya uchumi wa nchi. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa viwanda (pamoja na utoaji wa huduma za jamii) ulisababisha hali ambayo uzalishaji wa uwezo ulienda sambamba na kushuka kwa uwezo uliozalishwa.

Zaidi ya hayo, kipindi cha kuanzia mwaka 1967 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1980, Tanzania ililenga kujiondoa kutoka kutegemea misaada, hii ikiwa hatua nyingine kuelekea kwenye dhana ya kujitegemea. Mnamo miaka ya 1960 na 1970 misaada mingi ilikuja kwa mapatano ya pande mbili, na iliendana na ajenda na vipaumbele vya taifa. Kutokana na hali hiyo, misaada mingi katika miaka ya 1960 na mwanzoni mwa miaka ya 1970 ilikuwa inaelekezwa kwenye sekta za kilimo na usafiri. Na, wakati wa nusu ya pili ya miaka ya 1970 mkazo ukahamishwa kutoka kwenye kilimo hadi kwenye viwanda na nishati. Wafadhili—waliohusisha pande mbili na wale wa pande zaidi mbili—waliunga mkono mpango wa maendeleo ya Tanzania bila kuweka masharti yaliyoingilia sera zilizokuwapo. Licha ya kutegemea misaada kwa kiwango kikubwa, bado Tanzania ilibakia na hadhi, uhuru na umiliki wa ajenda ya maendeleo.

Hata hivyo, fungu la msaada kwenye miradi liliongezeka kwa kuwa fedha kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) zilipungua. Katika kipindi hicho kasi na mfululizo wa utekelezaji wa miradi vilielekezwa na kuwapo kwa misaada ya nje kuliko vipaumbele vya taifa. Katika miaka ya mwanzoni mwa 1980 fungu la misaada iliyohusisha mapatano ya pande nyingi liliongezeka, hii ilisababisha kuongezeka kwa masharti ya sera. Kadiri mdororo wa kiuchumi ulivyopamba moto mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980, matumizi ya mwongozo wa maendeleo wa kijamaa ulipata msukumo na shinkizo kubwa zaidi ili kubadili mwelekeo. Pamoja na serikali kukataa kabisa kubadili sera zake, anguko la mfumo wa kiuchumi pamoja kutoweza kutoa bidhaa na huduma vilizidi kudhoofisha kuaminika kwake. Mwaka 1986, wakati uhalali wa kisiasa kwa Serikali ulikuwa unaanza kuhojiwa, pamoja na kuongezeka kwa hatari ya kuangushwa, serikali ya Tanzania ilisalimu amri kwa shinikizo la kimataifa, na hatimaye, iliukubali Mpango wa Kurekebisha Muundo wa Uchumi kama sehemu ya Mkakati wa Kufufua Uchumi (1986-89).

Marekebisho na Mabadiliko ya Mfumo wa Kiuchumi (1986 hadi 1996)

Kipindi cha programu za mageuzi na marekebisho ya mifumo kuanzia mwaka 1986 hadi 1996 kilishuhudia kutenganishwa kwa sera za kiuchumi na za kijamii. Awamu ya kwanza ya mageuzi chini ya ERP (1986-89) ilijikita katika "ukadiriaji wa thamani halisi" kupitia ukombozi na mageuzi ya uchumi mkubwa, yakiwamo mageuzi ya sera ya biashara, kushushwa kwa thamani ya fedha, kuondolewa kwa udhibiti wa bei, pamoja na kuondolewa kwa ruzuku. Hii ilifuatiwa na awamu ya pili ya mageuzi ya kitaasisi katika mfumo wa maboresho ya utumishi wa umma, ubinafsishaji na utawala bora. Kwa upande wa sekta za kijamii, mageuzi yalienda sambamba na uanzishwaji wa uchangiaji wa gharama. Hii ilimaanisha kuwa kaya sasa zilitakiwa kuchangia sehemu ya gharama za huduma za jamii. Matokeo yake uanzishwaji huu wa kuchangia gharama ulisababisha watu maskini na makundi mengine ya pembezoni kunyimwa fursa ya kupata huduma kwa sababu wasingeweza kuchangia gharama.

Wakati mageuzi hayo yalipanua wigo wa kupata misaada ya ziada kutoka nje, mipango ya marekebisho ya uchumi ilipuuza madhara ya kijamii yanayotokana na mageuzi na mabadiliko hayo. Kimsingi, mageuzi hayo hayakuwa na mbinu zozote za kuwainua maskini na kuwawezesha kufaidi fursa muhimu katika uchumi wa soko. Zaidi ya hayo, utaratibu wa kifedha haukutoa njia endelevu za kufafanua matumizi ya umma yanayojali mahitaji ya maskini, kama vile kupata mahitaji muhimu. Pia, haukutengeneza fursa za kuwawezesha kupata huduma za umma pamoja na rasilimali kama vile ardhi na fedha ambazo huhitajika katika kusaidia uzalishaji mali.

Mantiki ya kuanzishwa kwa sera za Marekebisho ya Muundo wa Kiuchumi ilijikita katika kuboresha ukuaji wa kiuchumi pamoja na kuhakikisha mabadiliko ya kimfumo yanapewa kipaumbele katika kuzalisha mali kwanza kabla ya kuingiza katika matumizi ya jumla na ya jamii. Dhana kuu ya mpango huu ni kwamba, ili kuimarisha ukuaji, inabidi kujinyima kwenye mahitaji, hususani kupunguza gharama za serikali na matumizi ya kijamii. Sera ilikuwa inasukumwa na maafikiano ya kibiashara baina ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na baina ya usawa na ufanisi.

Kipindi hiki kilitawaliwa na viashiria vya uchumi dhaifu na kufifia kwa viashiria vya kijamii. Muongo mzima ulibakia kipindi cha giza hasa kuhusu ukuaji na utoaji wa huduma za jamii hadi ulipoanzishwa mpango wa kusamehe madeni makubwa kwa nchi maskini (Heavily-Indebted Poor Countries, HIPCs) mwaka 1996.

Kudai tena Udhibiti wa ajenda ya Maendeleo ya Taifa (1996-2016)

Katika kipindi cha karibuni (1996-2016), Serikali imejitahidi sana kudai tena udhibiti wa ajenda ya mageuzi ya kitaifa. Dira ya maendeleo ya muda mrefu ilianzishwa kama sehemu ya juhudi hizo ili kutoa mwongozo wa mwelekeo wa maendeleo ya nchi. Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya mwaka 2025 (The Tanzania Development Vision, TDV) na Dira ya Zanzibar ya mwaka 2020 (Zanzibar Vision 2020) zinajumuisha shauku ya nchi kufikia mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Ukosefu wa usawa na umaskini ni masuala muhimu kwenye dira zote mbili katika ukuaji wa kiuchumi ulio mkubwa na jumuishi. Kwenye elimu Kipaumbele kimewekwa katika jamii inayoendelea kujifunza ambayo utamaduni wa ubunifu, uvumbuzi na ujasiriamali vinahamasishwa na uboreshaji wa uwezo ili kuhimili ushindani.

Dira ya mwaka 2025 na ile ya mwaka 2020 ziliandaliwa ili zitekelezwe kupitia mipango ya miaka mitano mitano iliyoanza mwaka 2000. Hata hivyo, utekelezaji wake uliahirishwa ili kujadiliana na taasisi za fedha za kimataifa kuhusu kusamehewa madeni yanayohusiana na kupunguza umaskini. Hii ilifuatiwa na kuanzishwa kwa mfululizo wa makala za mkakati wa kupunguza umaskini (PRSPs). PRSP ya miaka ya 2000/01-2002/03, pamoja na awamu ya kwanza na ya pili ya Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini kwa Tanzania Bara (MKUKUTA I 2005/06-2009/10 na MKUKUTA II 2010/11-2014/15); pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Zanzibar (MKUZA I na II) (JMT 2005 na 2010). Makala hizi za mikakati ya kupunguza umaskini zilitokana na mwongozo makini wa maendeleo (Comprehensive Development Framework, CDF) uliandaliwa na Benki ya Dunia mwaka 1999. Mwongozo huu Makini wa Maendeleo ulidai kuwa ulizingatia vipengele vyote vya maendeleo—kijamii, kimfumo, kibinadamu, kiutawala bora, kimazingira, kiuchumi na kifedha, ukilinganishwa na marekebisho ya kwanza na ya pili ya kimfumo. Hata hivyo, ushiriki ulikuwa kikwazo katika utekelezaji wake, maudhui ya makala hizi yalimezwa na sekta ya kijamii kama nguzo muhimu ya kuondoa umaskini, kuondoa ukosefu wa usawa, na kuboresha fursa kwa watu.

Kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi 2015, kilishuhudia ukuaji mzuri wa kiuchumi nchini Tanzania, ambapo Pato la Ndani liliongezeka kwa wastani wa asilimia 6.6. Hata hivyo, bado kuna masuala ya msingi yanayopaswa kushughulikiwa; yaani kutofikiwa kwa kiwango cha ukuaji wa uchumi kilichotarajiwa, kutokuwapo kwa usawa, kasi ndogo ya kupunguza umaskini, pamoja na mageuzi madogo ya kiuchumi. Hoja hizi zikihusishwa na mapitio ya mwaka 2009 kuhusu utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, ziliishawishi Serikali kuamua kwamba wakati umefika wa kupanga mipango ya muda mrefu. Matokeo yake, ukaandaliwa Mpango wa Muda mrefu ya mwaka 2011/12–2025/26 (The Long Term Perspective Plan, LTPP), utakaotekelezwa kwa mipango mitatu ya miaka mitano mitano (FYDP). Kila mpango una eneo lake maalum la kutilia mkazo na vipaumbele. Mada kuu ya Mpango wa II wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17–2020/21) ambao unatekelezwa hivi sasa ni 'Kuendeleza Viwanda ili kufikia mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu'. Msukumo wa Mpango wa II wa Miaka Mitano unatoa fursa ya kuyafikia mageuzi ya kiuchumi (kupitia viwanda) yanayohusiana na maendeleo makubwa ya binadamu. Kwa sasa Zanzibar inaandaa mpango wa III wa MKUZA; unaotarajiwa kuwianisha sera za kiuchumi na kijamii ili kuifikia Dira ya Maendeleo ya mwaka 2020.

Kwa jumla, uchambuzi wa historia ya kufungamana kwa sera ya kijamii na kiuchumi nchini Tanzania tangu uhuru mwaka 1961 unaonyesha kuwa sera ya kiuchumi pekee hazitoshi kufikia kiwango cha maendeleo ya binadamu kinachotakiwa. Kinyume chake, malengo ya sera ya kijamii yanapaswa kuwa sehemu muhimu ya sera ya maendeleo; hii ni kama ilivyokubaliwa kimsingi na kujumuishwa katika Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano. Zaidi, ikiwa utekelezaji wa sera ya kijamii utafanywa kama "ziada tu" ya sera za kiuchumi kama ilivyotokea wakati wa marekebisho ya kiuchumi nchini Tanzania, kuna hatari ya kuwa ukuaji wa kiuchumi utakaoshindwa kuboresha hali ya maisha ya watu wengi. Kwa hiyo, kazi iliyobaki ni kusimamia uhusiano wa sera za kiuchumi na ya kijamii wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Miaka Mitano na baadae.

4.

Sera ya kijamii kama njia na lengo la mageuzi ya kiuchumi kwa maendeleo ya binadamu: Ujumbe muhimu katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya pili

Kama uchambuzi ulivyoonyesha kwenye ripoti ya Maendeleo ya Binadamu nchini Tanzania, 2017, maendeleo ya watu yamekuwa msingi wa sera yake ya maendeleo tangu uhuru, na hata katika miaka ya karibuni, Tanzania imepiga hatua kubwa katika viashiria muhimu vya maendeleo ya binadamu. Kwa kutumia kipimo cha umaskini kwa vigezo mbali mbali (MPI), Tanzania imepunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya watu wanaoishi katika umaskini kutoka asilimia 64 mwaka 2010 hadi asilimia 47 mwaka 2016. Zaidi ya hayo, kati ya 2007 na 2012, Tanzania imepunguza umaskini wa kipato kutoka asilimia 34.9 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 mwaka 2012. Matokeo haya yanayotia moyo ni ishara za awali za ukuaji rafiki wa kiuchumi kwa maskini.

Kwa ujumla, viashiria vya kipato, afya na elimu vimeboreshwa kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, uchambuzi wa taarifa mbalimbali unaonyesha tofauti kubwa katika maendeleo kimkoa, kimakazi (mjini dhidi ya vijijini) na hali ya mali kwa kaya. Kurudi nyuma kwa hivi karibuni katika viashiria vikuu vya elimu, baada ya muongo wa hatua za maendeleo, vikiunganishwa na idadi kubwa ya Watanzania waliofikia umri wa kuajiriwa kwa mwaka pia ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, serikali itahitaji kufuata dira ya maendeleo kwa dhati.

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti, ujumbe muhimu ufuatao unatolewa kwa ajili ya kuzingatiwa na watunga sera wa serikali na wadau wa maendeleo kwa ili kuyafikia mageuzi endelevu ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu.

Ujumbe Muhimu:

- **Mafanikio katika mapinduzi ya viwanda kwa maendeleo ya binadamu yanaweza kupatikana ikiwa malengo yatasawiri sera mwafaka ya jamii.**

  Labda changamoto muhimu ya kisera kwa serikali ya Tanzania ni kufafanua njia muafaka ya kufikia mapinduzi ya viwanda ili kukuza maendeleo ya binadamu. Kwa kuzingatia yaliyomo kwenye Mkakati wa Msingi wa Viwanda (1975-1995), inawezekana na inahitajika kuweka vipaumbele kwa mabadiliko ya kimuundo na kujitegemea, kwa kuimarisha viwanda vinavyokidhi mahitaji ya msingi ya watu (hususan afya, elimu na makazi) na kuzalisha bidhaa muhimu za viwandani, kama vile pembejeo za kilimo, magari na zana, vifaa vya umeme wa jua na baskeli katika maeneo ya vijijini, pamoja na ugavi, zana na vifaa vingine vya miradi midogo na ya kati kwenye maeneo ya mijini.

- **Mageuzi ya kilimo yanahitaji kuwekewa kipaumbele kikubwa katika ajenda ya maendeleo**

  Suala la mageuzi ya kilimo linabaki kuwa hoja kuu ya kufikia Tanzania ya Viwanda, kutokana na asilimia 70 ya watu kuishi maeneo ya vijijini. Mapinduzi ya viwanda yanayosaidia maendeleo ya binadamu yatahitaji kufungua fursa ya uzalishaji katika maeneo ya vijijini na kuongeza uhusiano kati ya sekta zinazotoa malighafi na zile zinazopelekewa kati ya kilimo, uzalishaji viwandani; na sekta ya huduma kama njia ya kupunguza umaskini vijijini.

- **Ukuaji wa uchumi unahitaji kufikiwa kwenye mazingira endelevu**

  Mpango wa Mandeleo wa Miaka Mitano awamu ya Pili unatambua kwamba ukuaji wa kiuchumi unatakiwa ufikiwe kwenye mazingira wezeshi na endelevu, kwa kusisitiza uchangamani wa masuala ya mazingira, pamoja na ya kiuchumi na kijamii. Uhusiano huu wa ziada ni wa muhimu sana. Upo ushahidi wa maandishi kwamba matumizi mabaya ya mali asili na uharibifu wa mazingira vinazuia ukuaji wa uchumi, unachochea umaskini wa namna tofauti kwa muda fulani, na kukwaza ufikiwaji wa malengo muhimu kama vile kupunguza umaskini na usalama wa chakula, hasa katika maeneo ya vijijini.

- **Ni lazima uwepo uwiano kati ya kujenga uwezo mpya wa uzalishaji (kupitia matumizi ya maendeleo) na kutumia vizuri uwezo wa sasa (kupitia matumizi ya kawaida).**

  Moja ya sababu kubwa ya mdororo wa kiuchumi katika miaka ya 1980 ilikuwa ukosefu wa uwiano katika mgawanyo wa rasilimali kwa miradi mipya na rasilimali za kuendeleza uwezo wa nchi katika uzalishaji. Hatari ya kurejea kwa ukosefu huu wa uwiano inahitaji kushughulikiwa kwa umakini mkubwa. Matumizi mazuri ya rasilmali zilizopo yanaweza kuangaliwa, ikiwa ni pamoja na matumizi ya vifaa vya gharama nafuu vya ujenzi, kwa mfano kwa kuwezesha juhudi zaidi za wananchi kujitolea.

- **Ili mabadiliko ya kiuchumi yaboreshe hali ya binadamu, mahitaji ya huduma za jamii kwa watu wanaoongezeka ni lazima yapangwe na taratibu ziwekwe ili kuimarisha tija ya kiuchumi kwa watu.**

  Mabadiliko ya masuala yanayohusiana na idadi ya watu, maendeleo ya nguvu kazi na maendeleo kijiografia vyote vina matokeo ya muda mfupi na mrefu kwenye sera ya maendeleo. Idadi ya watu nchini Tanzania inaongezeka kwa haraka, na kuhama kutoka vijijini kuja mijini kunatoa fursa nyingi lakini pia kuna changamoto za kiutawala katika ngazi zote. Hata hivyo, ubunifu uliofanywa wa sera changamani za kijamii na kiuchumi, inawezekana kuweka msawazo katika mtawanyiko wa watu katika nchi ili kuchipusha mageuzi ya kiuchumi.

  Ili ajenda ya serikali kuhusu mageuzi ya uchumi-jamii iwe jumuishi, ni muhimu kuwa na mwongozo wa kuchambua mipango mahususi ya maendeleo ya watu. Changamoto ya kukua haraka kwa miji na athari zake kijiografia zinahitaji pia umakini mkubwa katika kuandaa mipango ya vijijini na mijini na kuimarisha uhusiano kati ya vijiji na miji, kwa mfano, kwa kuanzisha kanda za kiuchumi.

- **Elimu ndio msingi wa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu**

  Ili kukuza maendeleo na faida inayotokana na fursa zinazoletwa na utandawazi na ushirikiano wa kikanda, Tanzania inatakiwa kuhakikisha watu wake wanaweza ushindani kwa kuwapatia vijana maarifa, ujuzi na uwezo unaofaa katika soko la ajira la dunia ya karne ya 21. Kama ilivyosisitizwa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili, mafanikio ya elimu yanatakiwa kuendelezwa kwa kuimarisha uongozi wa shule, ukaguzi na viwango. Upatikanaji wa ujuzi maalumu pia ni muhimu katika kuimarisha ushindani wa nguvu kazi ya taifa kwa jumla na kupata ujuzi mahususi unaotakiwa kwenye viwanda vya kipaumbele. Hii lazima itahusisha kubainisha ujuzi unaotakiwa, kutambua ujuzi mwafaka na mchanganyiko, na kushughulikia ujuzi usioendana kwa kuhakikisha mafunzo yanatolewa ni yanayohitajika wakati huo.

- **Sekta ya afya nchini Tanzania inaweza kuwa na tija zaidi kiuchumi na kijamii ikiwa sera ya afya na sera ya viwanda zitahusianishwa zaidi.**

  Sekta ya afya ni muhimu kiuchumi na kijamii kama sekta kuu ya huduma, ni sehemu ya kuwekeza, kuzalisha ajira na kipato, ni sekta ya mafunzo ya ujuzi na ajira, na kukuza viwanda pia. Kwa hiyo, kuimarisha uhusiano katika uchumi wa ndani kwa kina na upana, kati ya huduma za afya na watoaji huduma wa viwandani na wafanyabiashara kunaweza kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kuboresha huduma za afya. Kwa sasa, mahitaji ya dawa nchini Tanzania kwa kiwango kikubwa yanatoshelezwa kutoka nje ya nchi. Kwa hivyo, ripoti hii inapendekeza kipaumbele kiwekwe katika kusaidia viwanda vya ndani vinavyozalisha dawa na vifaa tiba, na kutumia sera za uingizaji baadhi ya bidhaa zinazolinda sekta hii. Hatua za makusudi zinahitajika ili manunuzi ya umma yafanywe kwa wazalishaji wa ndani na kuhamasisha wahisani kusaidia viwanda vya ndani kwa sekta ya afya.

- **Kuwajengea uwezo wanawake kuziba pengo la usawa wa kijinsia kwa ajili ya maendeleo ya binadamu**

  Fursa sawa ya elimu kwa wasichana na wanawake ni muhimu ili kupata usawa wa kijinsia, kupunguza vifo vya watoto, kupunguza ndoa za utotoni na kuzalisha viongozi wanawake. Katika miaka ya hivi karibuni, serikali imepiga hatua kubwa katika kuboresha fursa za elimu kwa wasichana, hususan katika shule za msingi na sekondari. Hata hivyo, wanawake bado ni wachache katika elimu ya juu, jambo linalowazuia kupata nafasi za juu za ajira na zenye malipo mazuri. Hivyo, kuondoa pengo la usawa wa jinsia katika elimu na ujuzi ni lazima vipewe kipaumbele sana. Wakati huohuo, wahamasishwe kusoma zaidi masomo ya sayansi ili kuwajengea uwezo thabiti kwenye soko la ajira. Mafunzo zaidi na maalumu yanatakiwa kutolewa na serikali, na waajiri, pamoja na mpango maalumu wa mafunzo kwa msaada wa wahisani mbalimbali yenye lengo la kutoa fursa zaidi kwa wanawake. Pia, kupanua hifadhi ya jamii ni njia ya uhakika ya kupunguza umaskini na ukandamizaji pamoja na kuziba pengo la jinsia; na hivyo kupata haki za msingi za wanawake na familia zao.

- **Sera na mipango jumuishi ya kijamii na kiuchumi inatakiwa kulenga makundi yaliyotengwa na kusahauliwa**

  Tofauti ya kipato, mali na fursa mbalimbali yalikuwa ni masuala makuu katika kipindi baada ya uhuru miaka ya 1960 nchini Tanzania. Leo, jamii ya Tanzania bado inazo tofauti kubwa miongoni mwa makundi ya kijamii, jambo linalohitaji kushughulikiwa katika mchakato wa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu. Katika ngazi ya kisera, serikali itatakiwa kupata na kutumia taarifa mbalimbali ili kuwatambua na kuwalenga watu walioachwa nyuma. Sera na mipango itatakiwa kujumuisha hifadhi ya jamii yenye tija ili kuondoa umaskini (kwa mfano, kwa kuhusianisha shughuli za umma na maisha) na kuchangia mageuzi mwafaka. Jitihada za kuwa na usawa wa kijinsia lazima zifanywe kipaumbele mahsusi ili kufikia maendeleo jumuishi.

- **Serikali ina jukumu la kimkakati katika mageuzi ya kitaifa**

  Uzoefu unaonyesha kwamba hata nchi zilizofanikiwa hazikupata mageuzi ya kiuchumi kwa kutegemea tu nguvu za soko huria. Bali serikali zilikuwa na wajibu muhimu wa kuhakikisha kwamba ukuaji wa uchumi unaleta mageuzi bora ya kijamii. Kwa kuachana na sera zake wakati kipindi cha marekebisho ya uchumi, Serikali ya Tanzania iliacha jukumu lake katika mabadiliko ya uchumi. Hivyo, katika kipindi kijacho, Serikali itatakiwa kufanya mkakati wa kusimamia nguvu za soko, kushughulikia udhaifu wa soko, kutoa bidhaa muhimu zinazotegemewa na soko, kuhimili uchumi mkubwa, na kutekeleza sera zinazoboresha mazingira ya biashara. Pia, muundo wa kitaasisi utahitajika ili kuhakikisha kwamba sekta au wizara mbalimbali hazifanyi kazi kila moja peke yake bali kama kitu kimoja.

- **Utashi wa kisiasa, uongozi thabiti, na umiliki wa jamii ni muhimu ili kupata mageuzi endelevu ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu.**

  Uzoefu wa kipindi kilichopita unaonyesha kwamba utashi wa kisiasa na uongozi wenye dhamira ya dhati ni muhimu ili kupata mageuzi ya kiuchumi pamoja na maendeleo ya binadamu. Kimsingi uongozi wenye mtazamo na dhamira wa Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanzania, ulisisitiza maendeleo ya watu katika muundo wa sera ya taifa na ulikuwa na uwezo wa kushawishi viongozi na wadau wengine kutekeleza mipango ya maendeleo. Vivyo hivyo, jitihada za karibuni za serikali ya Tanzania kuhamasisha jamii kushiriki na kumiliki mipango ya maendeleo zinatia matumaini, aidha mchakato wa kuhamasisha wananchi kusaidia juhudi za serikali katika maeneo wanayoishi, zinatakiwa zitaasisishwe ili ziwe endelevu zaidi.

Hitimisho

Kama uchambuzi wa ripoti hii ulivyoonyesha, Tanzania ina nafasi kubwa ya kujifunza kutokana na uzoefu wake wa maendeleo pamoja na wa nchi nyingine ambazo zimeunganisha malengo yake ya kiuchumi na sera ya jamii ili kuyafikia mageuzi ya kimuundo. Kimsingi, katika nchi zilizofanikiwa serikali imeshiriki katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unaleta matokeo tarajiwa kwa jamii husika.

Jambo muhimu ni kwamba mbinu zilizotumika zilikuwa jumuishi na shirikishi; michakato mbalimbali ilitumika ili kuhakikisha kwamba huduma za jamii zililenga idadi kubwa ya watu na taratibu kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi yaliyolenga kushirikisha wananchi wote. Viwango vya juu vya matumizi kwenye huduma za msingi za jamii viliendelezwa, na kuhusianishwa na shughuli za uzalishaji. Mafanikio haya yanaonyesha kwamba mageuzi ya kimuundo yanayokwenda sambamba na viwango vya juu vya maendeleo ni mambo yanayowezekana ikiwa vipaumbele vya kiuchumi na kijamii vinafungamanishwa kwa usahihi na rasilimali zinagawanywa kimkakati na kwa ufanisi.

Pengine, jambo la muhimu zaidi, maendeleo yanayolenga watu yalikuwa msingi katika kuandaa sera za serikali katika kipindi cha baada ya uhuru wa Tanzania. Sera zote zilikuwa na malengo mawili, ikijumuishwa na ule Mkakati wa Kiwanda vya Msingi, ilikuwa kuyafikia mabadiliko ya kimuundo pamoja na kujitegemea. Kwa msingi huo, Mpango wa Miaka Mitano wa sasa unarejelea madhumuni haya mawili ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na kuboresha maendeleo ya binadamu nchini Tanzania. Kutokana na kuhusianisha vipaumbele vya kijamii na kiuchumi sambamba na mazingira, mpango unaakisi Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030.

Marejeleo

Agwanda, A. and H. Amani. 2014. "Population Growth, Structure and Momentum in Tanzania." THDR 2014: Background Paper No. 7, ESRF Discussion Paper 61. Economic and Social Research Foundation, Dar es Salaam.

Aikaeli, J., and H. Moshi. 2016. "Social policy in a historical perspective: Shifting Approaches to Social Provisioning." THDR 2017: Background paper No. 6. ESRF, Dar es Salaam.

Amani, H, T. Kida, and D. Sango. 2016. "The Status and Progress of Human Development in Tanzania Mainland". THDR 2017: Background paper No. 1. ESRF, Dar es Salaam.

ESRF, United Nations Development Programme (UNDP) and Ministry of Finance [URT] (MOF). 2015. "The Tanzania Human Development Report 2014: Economic Transformation for Human Development." ESRF, Dar es Salaam.

Kessy, F., and M. Omar. 2016."Status and Progress in Human Development in Zanzibar." THDR 2017: Background paper No. 2, ESRF Discussion Paper 64. ESRF, Dar es Salaam.

Kessy, F., and R. Mahali. 2016. "Water, Sanitation, and Hygiene Services in Tanzania: Access, Policy Trends and Financing." THDR 2017: Background paper No. 11. ESRF, Dar es Salaam.

Lokina, R., J. Nyoni and G. Kahyarara. 2016. "Social Policy, Gender and Labour in Tanzania." THDR 2017: Background paper No. 7. ESRF Discussion Paper 68. ESRF, Dar es Salaam.

Mackintosh, M., and P. Tibandebage. 2016. "Health as a Productive Sector: Integrating Health and Industrial Policy." THDR 2017: Background paper No. 8, ESRF Discussion Paper 69. ESRF, Dar es Salaam.

MoHCDGEC (Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children) [Tanzania Mainland], Ministry of Health (MoH) [Zanzibar], National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS) and ICF. 2016. "Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MIS) 2015–16." Dar es Salaam, Tanzania, and Rockville, Maryland, USA: MoHCDGEC, MoH, NBS, OCGS and ICF.

Myamba, F., and S. Kaniki. 2016. "Social Protection: Safety Net or Vehicle for Transformation?" THDR 2017: Background paper No. 9. ESRF Discussion Paper 70. ESRF, Dar es Salaam.

NBS and ICF Macro. 2011. "Tanzania Demographic and Health Survey 2010." Dar es Salaam, Tanzania: NBS and ICF Macro.

Nyerere, J. K. 1967. Socialism and Rural Development. Government Printer, Dar es Salaam.

_____. 1968. Education for Self-Reliance. Oxford University Press, Dar es Salaam.

_____. 1973. Freedom and Development. Oxford University Press, Dar es Salaam.

OCGS (Office of the Chief Government Statistician [Revolutionary Government of Zanzibar]). 2012. "Household Budget Survey 2009/10 (Final Report)." Zanzibar, OCGS.

_____. 2016. "Household Budget Survey 2014/15: Income and non-income poverty preliminary results." Zanzibar, OCGS.

OPHI (Oxford Poverty and Human Development Initiative). 2013. "Tanzania Country Briefing." Multidimensional Poverty Index Data Bank, University of Oxford www.ophi.org.uk/multidimensionalpoverty-index/mpi-country-briefings

Otieno, A.A., H.K. Amani and A. Makbel. "Population Dynamics and Social Policy." THDR 2017: Background Paper No. 3, ESRF Discussion Paper 65. Economic and Social Research Foundation, Dar es Salaam.

RGoZ (Revolutionary Government of Zanzibar). (2000). "Zanzibar Development Vision 2020." President's Office, Planning and Investments.

_____. 2010. "Zanzibar Strategy for Growth and Reduction of Poverty (ZSGRP II) 2010–2015 (MKUZA II)." President's Office, Finance, Economy and Development Planning, RGoZ.

Sen, A. 1999. Development as Freedom. Oxford University Press, Oxford, U.K.

Sumra, S., and J. Katabaro. 2016. "Education Foundations of the Development of Skills and Productive Capabilities." THDR 2017: Background paper No. 10, ESRF Discussion Paper 71. ESRF, Dar es Salaam.

TACAIDS (Tanzania Commission for AIDS), Zanzibar AIDS Commission (ZAC), National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS), and Macro International Inc. 2008. "Tanzania HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey 2007-08." Dar es Salaam, Tanzania: TACAIDS, ZAC, NBS, OCGS, and Macro International Inc.

TACAIDS (Tanzania Commission for AIDS), Zanzibar AIDS Commission (ZAC), National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS), and ICF International. 2013. "Tanzania HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey 2011–12." TACAIDS, ZAC, NBS, OCGS and ICF International, Dar es Salaam.

TANU (Tanganyika Africa National Union). 1967. The Arusha Declaration and TANU's Policy on Socialism and Self-Reliance. Publicity section, TANU, Dar es Salaam.

UNDP (United Nations Development Programme). 1990. Human Development Report 1990: Concept and Measurement of Human Development. Oxford University Press, New York http://hdr.undp.org/sites/default/files/reports/219/hdr_1990_en_complete_nostats.pdf

_____. 1995. Human Development Report 1995: Gender and Human Development. Oxford University Press, New York. http://hdr.undp.org/sites/default/files/reports/256/hdr_1995_en_complete_nostats.pdf

_____. 2001. Human Development Report 2001: Making New Technologies Work for Human Development. Oxford University Press, New York. http://hdr.undp.org/en/content/human-development-report-2001

_____. 2010. Human Development Report 2010: The Real Wealth of Nations: Pathways to Human Development. Palgrave Macmillan, New York.

_____. 2016. Human Development Report 2016: Human Development For Everyone. UNDP, New York.

UN Women. 2015. "Progress of the World's Women 2015-2016: Transforming Economies, Realizing Rights." UN Women, New York.

URT (United Republic of Tanzania). 1999. "The Tanzania Development Vision 2025." Planning Commission, Dar es Salaam.

_____. 2005. "National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (MKUKUTA I)." Ministry of Planning, Economy and Empowerment, Dar es Salaam.

_____. 2006. "Tanzania 2002 Census Analytical Report vol. X." National Bureau of Statistics (NBS), Ministry of Planning, Economy and Empowerment, Dar esSalaam.

_____. 2009. "Household Budget Survey 2007 – Mainland Tanzania. NBS, Dar es Salaam.

_____. 2010. "National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (MKUKUTA II)." Ministry of Finance and Economic Affairs, Dar es Salaam.

_____. 2012. "The Long Term Perspective Plan LTPP 2011/12–2025/26: The Roadmap to Middle Income Country." President's Office, Planning Commission (POPC), Dar es Salaam, Tanzania.

_____. 2013a. "The 2012 Population and Housing Census Population: Distribution by Age and Sex." NBS, Dar es Salaam and Office of Chief Government Statistician, President's Office, Finance, Economy and Development Planning, Zanzibar

_____. 2013b. "The 2012 Population and Housing Census: Population Distribution by Administrative Units—Key Findings." National Bureau of Statistics (NBS), Dar es Salaam and Office of Chief Government Statistician (OCGS), Zanzibar.

_____. 2014a. "Household Budget Survey 2011/12 – Main Report." NBS, Dar es Salaam.

_____. 2014b. "The 2012 Population and Housing Census: Basic Demographic and Socio-Economic Profile—Key Findings." National Bureau of Statistics (NBS) and Office of Chief Government Statistician (OCGS) Zanzibar.

_____. 2015a. "Mortality and Health Monograph: 2012 Tanzania Population and Housing Census." NBS, Dar es Salaam and OCGS, Zanzibar. http://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/census2012/Mortality_and_Health_Monograph.pdf

_____. 2015b. "Fertility and Nuptiality Monograph: 2012 Population and Housing Census." NBS, Dar es Salaam and OCGS, Zanzibar.

_____. 2015c. "Literacy and Education Monograph: 2012 Population and Housing Census." NBS, Dar es Salaam and OCGS, Zanzibar.

_____. 2015d. "Migration and Urbanization Monograph: 2012 Population and Housing Census." NBS, Dar es Salaam and OCGS, Zanzibar.

_____. 2015e. "Integrated Labour Force Survey 2014—Analytical Report." National Bureau of Statistics, Dar es Salaam.

_____. 2015f. "Region and District Poverty Estimates for Tanzania, 2012." Poverty Eradication Division, Ministry of Finance and Planning, Dar es Salaam.

_____. 2016a. "National Five Year Development Plan 2016/17–2020/21." Ministry of Finance and Planning, Dar es Salaam.

_____. 2016b. "National Accounts of Tanzania Mainland 2007–2015." NBS, Dar es Salaam.

_____. 2016c. "Basic Education Statistics in Tanzania: Pre-primary, primary and secondary basic education statistics in brief." President's Office, Regional and Local Government Administration, Dar es Salaam.

_____. 2016d. "Basic Education Statistics in Tanzania: Regional data. President's Office, Regional and Local Government Administration, Dar es Salaam.

World Bank. 2015. "Tanzania Poverty Assessment." World Bank, Washington, D.C. https://openknowledge.worldbank.org/handle/10986/21871

Wuyts, M. and B. Kilama. 2014. "Economic Transformation in Tanzania: Vicious or Virtuous Circle?" THDR 2014: Background Paper No. 2, ESRF Discussion Paper 56. Economic and Social Research Foundation, Dar es Salaam.

Wuyts, M. and H. Gray. 2016. "Situating Social Policy in Economic Transformation: A Conceptual Framework." THDR 2017: Background papers No. 4, ESRF Discussion Paper 66. ESRF, Dar es Salaam.

Wuyts, M., D. Mushi, and T. Kida. 2016. "Aid Dependency in Financing the Space for Social Provisioning in Tanzania: A Macroeconomic Perspective." THDR 2017: Background paper No. 5; ESRF Discussion Paper 73. ESRF, Dar es Salaam.

Empowered lives.
Resilient nations.

United Republic of Tanzania

ESRF
Implementing Partner

Katika zama hizi, maendeleo ya Tanzania yanachagizwa na mikakati mikubwa mitatu: yaani, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Mpango wa Muda Mrefu wa 2011/12 – 2024/25 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Lengo hasa la mikakati hii ni kuhakikisha kwamba mpaka kufikia mwaka 2025, Tanzania inakuwa nchi ya kipato cha kati, ikiwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya binadamu na pato la mwaka la zaidi ya dola 3,000 za Marekani kwa kila mtanzania. Kielelezo kikuu cha maendeleo ya Tanzania katika kipindi hiki kitakuwa mageuzi ya kiuchumi kutoka uchumi unaotegemea kilimo chenye tija ndogo hadi uchumi wa kati unaotegemea viwanda, ukiambatana na sekta muhimu na inayokua kwa kasi ya huduma.

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2017 ni ya pili katika ya kitaifa kwa Tanzania. Dhima ya ripoti hii Sera ya Kijamii Katika Muktadha wa Mageuzi ya Kichumi – dhima ambayo ilichaguliwa mahsusi ili kujenga katika mawazo ya ripoti iliyotangulia yaani THDR 2014. Msingi mkuu wa THDR 2014 ulikuwa kwamba ili mageuzi ya kiuchumi yaweze kufanikisha maendeleo ya binadamu, ni muhimu kwa mchakato huu uende sambamba na utengenezaji wa ajira, ukuzaji wa kipato na utoaji wa huduma za kijamii. THDR 2017 inajenga katika ripoti iliyotangulia kwa kuchambua nafasi ya sera za kijamii na utoaji huduma katika mchakato unaoendelea wa mageuzi ya kiuchumi nchini Tanzania.

".....mageuzi ya kiuchumi yanayolengwa na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 ni mchakato unaoongozwa na sekta ya viwanda, unaolenga katika kujenga uchumi wenye kuhimili ushindani na kupelekea Maendeleo ya Binadamu. Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa ndio mwongozo wa kuyafikia mageuzi haya ya kiuchumi pamoja na kujenga jamii ambayo wananchi wake wote wanashiriki kikamilifu katika mchakato wa maendeleo. Mpango wa pili wa Maendeleo wa Taifa unafanya hivi kwa kuonanisha ujenzi wa viwanda na ukuzaji wa rasilimali watu"

Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa, ukurasa wa 37, Sura ya Kwanza

".....katika muktadha wa maendeleo, hakuna shaka kwamba nafasi ya sera za kijamii katika mataifa yanayoendelea inabidi ipewe msisitizo mkubwa zaidi ya vile zinavyopewa katika mataifa yaliyoendelea. Vile vile, ni muhimu pia sera za kijamii zitazamwe kama nyenzo ya kubadilisha kabisa hali za kiuchumi za wananchi na wala sio kwa mtazamo wa kuwapunguzia tu wananchi madhira ya umaskini bila kuwakomboa moja kwa moja"

~ Mkandawire, Sura ya 3

".....maendeleo yasitazamwe tu kama mchakato wa ulimbikizaji mali yaani kukuza pato la taifa uwezo wa taifa bali kama mageuzi ya kitaasisi katika muundo wa jamii. Hivyo basi, Maendeleo ya Tanzania yanahitaji kuanzishwa kwa shughuli ambazo zinalenga katika kuipatia jamii mahitaji ya msingi (chakula, makazi, afya, elimu, mawasiliano na uchukuzi) yakizingatia pia nafasi ya ubunifu wa wananchi na utunzaji wa mazingira"

~ Rweyemamu, Sura ya 3

www.thdr.or.tz